# Nipashe

Jumamosi Juni 29, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581722

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710 LIKE & FOLLOW US


**Padri** na wenzake wanane kizimbani shtaka la kumuua mwenye ualbino

UKURASA 4

**KUCHELEWESHA MAFAO**

Majaliwa aagiza waajiri wanaokiuka wajibu washtakiwe

UKURASA 3

**Nyanduga** akosoa sera kupendelea zaidi wanyamapori kuliko binadamu

UKURASA 2



**RAYVANNY HAWEZEKANI TENA**

UKURASA 12



HOJA ZA WAWEKEZAJI

# Serikali yawaita mabalozi watete

UKURASA 2

UKURASA WA 24

**YANGA YAFUNGA USAJILI MPYA, PACOME KUONGEZWA MKATABA**

## 20,000 watibiwa katika Kliniki ya Makonda Arusha

UKURASA 5



Sehemu ya umati wa wananchi waliojitokeza katika kambi ya matibabu bure iliyoandaliwa na Mkuu wa Mkoa wa Arusha, Paul Makonda kwa kushirikisha madaktari bingwa katika Uwanja wa Sheikh Amri Abeid, jijini Arusha jana. **PICHA: BEATRICE SHAYO**



Mwenyekiti wa Chadema Taifa, Freeman Mbowe akihutubia wananchi wa Katesh, wilayani Hanang mkoani Manyara jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mbowe atamba CHADEMA inachukua uongozi wa nchi

• **Lema** ulevi wa kupindukia unatesa nchi ... *Ukurasa 4*

**MICHEZO** **SIMBA DAY KUVUNJA REKODI MSIMU HUU** UK.24 **MAONI,** UK.6



Wazoa taka wakiwa kazini eneo la Sinza Makaburini, Dar es Salaam jana, huku wengine wakiwa hawana vifaa vya kujikinga mikononi kama 'gloves', kitendo ambacho ni hatari kwa usalama wa afya zao. **PICHA: SABATO KASIKA**

HOJA ZA WAWEKEZAJI

# Serikali yawaita mabalozi watete

**Na Mwandishi Wetu**

MABALOZI 10 nchini wameomba mkutano wa dharura na mawaziri watatu wa Tanzania kwa lengo la kutatua changamoto za uwekezaji zilizojitokeza, serikali imewakubalia.

Hao ni pamoja na Michael Battle anayewakilisha Marekani nchini, David Concar (Uingereza), Wiebe de Boer (Uholanzi), Nabil Hajlaoui (Ufaransa), Peter Hughebaert (Ubelgiji), Kyle Nunas (Canada) na Charlotta Macias (Sweden).

Wengine ni Thomas Terstegen (Ujerumani), Seungyun Lee (Korea) na Mags Gaynor anayewakilisha Ireland nchini.

Serikali ya Tanzania kupitia Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, January Makamba, imeahidi kuzifanyia kazi kwa haraka changamoto zinazokumba wawekezaji wa kigeni nchini ambazo zimeainishwa na mabalozi hao.

Miongoni mwa mambo waliyotaja mabalozi hao kupitia barua yao ya pamoja ya Juni 26 mwaka huu, ni wasiwasi kuhusu utaratibu wa usimamizi wa kodi unaofanywa na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kwa wawekezaji wa kigeni, wakitaka serikali kuingilia kati.

Katika barua yao hiyo, mabalozi wameomba kukutana na Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki mwenyewe, Waziri wa Fedha, Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais -Uwekezaji na Mipango, Waziri wa Viwanda na Biashara na Kamishna Mkuu wa TRA ili kujadili namna ya kutatua vikwazo vinavyolalamikiwa na wawekezaji kutoka mataifa yao.

Akijibu barua yao juzi, Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, January, amekubali kuzungumza nao, akisema serikali inaheshimu utawala bora na wa kisheria kama nguzo muhimu za maendeleo na ustawi.

"Tunajivunia kuwa na utawala wa kisiasa na kiuchumi ambao unavutia uwekezaji na kuwezesha maendeleo ya sekta binafsi.

"Ili mkutano huo uwe na tija, ninaomba wawekezaji unaowarejelea waandae muhtasari/uwasilishaji unaoelezea kwa uwazi, malalamiko yao," alisema Waziri January akimjibu Balozi wa Ufaransa nchini, Nabil Hajlaoui, aliyeandika barua hiyo kwa niaba ya mabalozi wenzake.

Waziri huyo alisema mafanikio ya kuvutia uwekezaji wa moja kwa moja kutoka nje (FDI) ndani ya Tanzania katika kipindi cha miaka mitatu iliyopita, yanathibitisha imani ambayo jumuiya ya kimataifa ya uwekezaji inayo kwa Tanzania.

"Ningependa kuwahakikishia kuwa serikali hii inachukua kwa uzito mkubwa ukiukwaji wowote unaodaiwa kufanywa na taasisi yoyote ya umma, ambayo inahatarisha mafanikio ya biashara yoyote katika nchi yetu na sifa yetu kama kivutio rafiki kwa wawekezaji," alisema January.

**YALIYOMO**

Katika barua yao ya Juni 26 mwaka huu, mabalozi hao wanashauri serikali kuzingatia umuhimu wa kujibu mapema suala hilo la dharura kama walivyoomba.

Wanasema mafanikio makubwa katika kuvutia na kupanua uwekezaji wenye ubora wa kimataifa nchini katika kipidi cha miaka michache iliyopita yanakabiliwa na usumbufu mkubwa kutokana na notisi zisizo na ushahidi kutoka TRA zinazodai malipo na masuluhisho ya akaunti yaliyowataka walipe madai hadi ya miaka 15 iliyopita. Kwa mujibu wa mabalozi hao, usajili wa uwekezaji wa biashara uliongezeka kutoka Dola za Marekani bilioni tatu mwaka 2022 hadi Dola za Marekani bilioni 5.5 mwaka 2023, jambo linaloonesha ushirikiano mzuri kati yao na Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC).

"Wawekezaji pia wanaripoti kuwa mawakala wa TRA hutoza bili zisizo za kawaida za kodi zisizoungwa mkono na sheria za Tanzania, hivyo kutishia wawekezaji na washirika wa Tanzania.

"Pale kampuni zinapopinga au kukata rufani dhidi ya vitendo hivyo, zinatishiwa kufungiwa au kukamata akaunti za benki na mali za kampuni," mabalozi hao wanadai katika barua yao hiyo.

Mabalozi hao wanasema wameendelea kujizatiti kufanya kazi kwa ushirikiano na Serikali ya Tanzania katika kutafuta suluhu za changamoto hizo zinazokwenda sambamba na kujenga upya imani katika mazingira ya biashara ya Tanzania, sambamba na azma ya nchi kufikia ukuaji uchumi jumuishi na kuwa miongoni mwa nchi zenye kipato cha kati.

## Nyanduga: Sera ya Uhifadhi inawajali zaidi wanyamapori

**Na Halfani Chusi**

KITENDO cha Sera ya Uhifadhi kumpa kipaumbele mnyama kuliko binadamu kimetajwa kuwa ni moja ya sababu za uvunjifu wa haki za binadamu hususani kwa wanaopakana na hifadhi za taifa.

Hayo yalisemwa jana jijini Dar es Salaam na Mwenyekiti mstaafu wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, Wakili Mwandamizi Bahame Nyanduga wakati wa uzinduzi wa ripoti ya masuala ya uhifadhi na haki za binadamu.

Ripoti hiyo ni matokeo ya utafiti na uchunguzi uliofanyika nchi nzima kuhusiana na madhila ya mara kwa mara yanayowafika wanaoishi karibu na hifadhi za taifa na kushauri hatua za kuchukua.

Wakili Nyanduga alisema kwa kushirikiana na wadau wengine, wameamua kufanya utafiti huo kutokana na kuwapo malalamiko ya ukiukwaji haki za binadamu kwa wanaoishi jirani na hifadhi.

Alisema lengo lao, pamoja na mambo mengine, ni kuonesha namna haki za binadamu zinavyokiukwa na Jeshi la Polisi pale serikali inapotekeleza masuala ya uhifadhi.

"Ninakubali na ninatambua umuhimu wa hifadhi, lakini ninapendekeza uhifadhi endelevu. Ukiangalia sera na taratibu, nyingi zimewalenga wanyamapori au misitu na kusahau binadamu.

"Kuna haja kuelimisha wananchi kuhusu hifadhi, kuzingatia sheria hasa pale panapokuwa na mjadala katika kuelewa sheria ili pasiwe na marudio ya hizi changamoto za mara kwa mara," alishauri Wakili Nyanduga.

Ofisa Mtendaji Mkuu Brain Media, Jesse Kwayu, alisema jamii zinazoishi karibu na hifadhi zinakumbwa na madhara mengi, ikiwamo kuteswa, kupigwa, kuuliwa na kunyang'anywa mali zao.

Alisema matukio mengine katika ripoti hiyo yanatisha, akigusia kuwa zipo simulizi za waliopoteza ndugu zao na kuporwa mali zao.

Kwayu alisema kuna haja kuwa na mkutano wa kitaifa wa kujadili masuala hayo ya uhifadhi na haki za binadamu.

Akisimulia namna alivyopata madhara kwa kuishi jirani na hifadhi katika Kijiji cha Ulukugwado, mkoani Arusha, Angelina Nassari alisema:

"Mwaka 2017, kijijini kwetu walikuja watu wa hifadhi na Jeshi la Polisi, walitufuata na kutuuliza 'kwanini mnaishi hifadhini?' Walikuwa wengi wakaanza kuturushia mabomu ya moshi na kututimua.

"Walirudi tena katika eneo tunalootesha mazao, wakasema ndani ya saa 24 hawataki kuona mtu katika eneo tunamoishi, wakapiga mabomu, wakaua mbuzi na ng'ombe wangu.

"Kule nilikotokea tunateseka sana, tunaishi kama bundi, hakuna taarifa wala ushirikishwaji wowote, ukiuliza wanakwambia ni uamuzi kutoka ngazi za juu, maana kule tunaishi kama wakimbizi."

Angelina aliomba serikali iangalie namna ya kuwasaidia ili waishi kwa amani kama ilivyo kwa raia wengine wasiopakana na hifadhi.

Mwathirika mwingine anayeishi jirani na Pori la Akiba Selou mkoani Lindi, Kasimu Mkwanga, alisema wakazi wa eneo hilo wanaishi kwa hofu kwa kile alichodai kipande walichopewa waishi kwa muda baada ya kuhamishwa kwa kupigwa na mabomu ya moshi na risasi pia, walivunja nyumba zetu na hatujalipwa chochote tangu siku hiyo mpaka leo (jana)," alisimulia.

"Jambo hili linatuacha njiapanda, hatujui nini cha kufanya, tukikumbuka tulipokuwa tunaishi mwanzo, tulihamishwa kwa kupigwa na mabomu ya moshi na risasi pia, walivunja nyumba zetu na hatujalipwa chochote tangu siku hiyo mpaka leo (jana)," alisimulia.

Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kwa mwaka 2021/22, ina taarifa kuhusu madhila ya watu wanaoishi karibu na hifadhi, ikijumuisha matukio ya kuuliwa na kujeruhiwa na wanyamapori.

KUCHELEWA KULIPA MAFAO

# 'Waajiri wanaokiuka wajibu wao washitakiwe'

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa ameitaka mifuko ya hifadhi ya jamii kuchukua hatua dhidi ya waajiri wote wanaokiuka kwa makusudi wajibu wao wa kuwasilisha michango ya wanachama kwa wakati.

Majaliwa alitoa agizo hilo jana bungeni jijini Dodoma wakati akitoa hoja ya kuahirisha mkutano wa 15 Bunge. Bunge limeahirishwa hadi Agosti 27 mwaka huu.

"Bodi na menejimenti za mifuko tumieni vifungu vya sheria katika kuhakikisha michango inawasilishwa kwa wakati ili kuwaondelea wastaafu changamoto za kulipwa mafao kwa kuchelewa," aliagiza Majaliwa.

Waziri Mkuu alisema kuwa katika kuhakikisha wastaafu wanalipwa kwa wakati, sheria za mifuko zinaelekeza mwajiri kuwasilisha taarifa ya maandishi katika mfuko ndani ya miezi sita kabla ya mtumishi kustaafu, ili mfuko uweze kuanza taratibu za kuandaa mafao ya mwanachama.

Alisema mifuko nayo inatakiwa ndani ya siku 60 baada ya mwanachama kustaafu iwe imeshamlipa mafao yake kama madai yake yatakuwa hayana kasoro na michango imewasilishwa kwa ukamilifu.

Alisema katika kipindi cha mwaka 2023/24, asilimia 90 ya madai ya wastaafu yamelipwa ndani ya muda wa siku 60 kwa mfuko wa NSSF na asilimia 61 kwa mfuko wa PSSSF.

"Sababu za baadhi ya wastaafu kutolipwa kwa wakati ni pamoja na michango yao kucheleweshwa kuwasilishwa katika mifuko na baadhi ya wastaafu kubadilisha kumbukumbu za utumishi kama vile tarehe ya kuzaliwa, majina na muda wa kuanza kazi," alisema.

Majaliwa alisema ili kukabiliana na tatizo la ucheleweshaji michango kutoka kwa waajiri, serikali imewasilisha Muswada wa Marekebisho ya Sheria za Mifuko unaolenga kuzipa nguvu Bodi za Wadhamini za Mifuko kupunguza au kusamehe kabisa tozo zinazotokana na ucheleweshaji michango.

Alisema marekebisho hayo yatawezesha waajiri wenye malimbikizo makubwa ya michango kulipa madeni yao na kuhakikisha wastaafu wanalipwa kwa wakati baada ya kulitumikia taifa lao.

"Nitoe rai kwa waajiri wote kuhakikisha wanalipa michango ya watumishi wao kwa wakati na kuondoa usumbufu wa kucheleweshwa kulipwa kwa watumishi hao pindi wanapostaafu.

"Niitake pia mifuko kuchukua hatua kwa waajiri wanaokiuka kwa makusudi wajibu wao wa kuwasilisha michango kwa wakati," Waziri Mkuu aliagiza.

Majaliwa pia alisema serikali inaboresha mazingira ya biashara na uwekezaji nchini kwa kutekeleza afua mbalimbali za kikodi na kiutendaji.

Hata hivyo, alisema kumekuwa na changamoto ambazo zimeendelea kujitokeza na kusababisha taharuki na sintofahamu nyingi hasa kwa wafanyabiashara nchini.

"Sintofahamu hizo kama ambavyo waheshimiwa wabunge walivyochangia humu bungeni katika siku za hivi karibuni ni pamoja na migomo ya wafanyabiashara wetu kutoka katika maeneo tofauti tofauti nchini," alisema.

Majaliwa alisema sehemu kubwa ya madai ya wafanyabiashara inatokana na hoja takribani 41 ambazo ziliwasilishwa na viongozi wa Jumuiya ya Wafanyabiashara Tanzania (JWT).

Alisema kati ya hizo, hoja sita zilikuwa za kisera na kisheria na zilizobaki 35 ni za kiutendaji ambapo serikali imefikia mwafaka katika kutatua kero zao.

"Serikali kwa pamoja na uongozi wa Jumuiya ya Wafanyabiashara nchini tumeafikiana kusimamia maazimio kama yalivyowasilishwa na Msemaji Mkuu wa Serikali.

"Nitumie fursa hii mbele ya Bunge lako Tukufu kuziagiza mamlaka zote za serikali kuhakikisha maazimio yote yanatekelezwa kwa ufasaha na kwa wakati uliokubalika na pande zote (yaani muda mfupi, muda wa kati na muda mrefu)," alisema.

Waziri Mkuu pia alisema serikali imekamilisha maandalizi ya uratibu wa upelekaji fedha za mikopo ya asilimia 10 katika mamlaka za serikali za mitaa kwenda mfuko wa mikopo ya vikundi na kusimamia urejeshwaji wa mikopo iliyotolewa miaka ya nyuma.

"Itakumbukwa kwamba mwezi Aprili 2023, serikali ilisitisha utoaji mikopo hii kwa ajili ya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu.

"Hadi kufikia mwishoni mwa mwaka huu wa fedha 2023/24, serikali imekamilisha maandalizi ya uratibu wa upelekaji fedha hizo katika mamlaka za serikali za mitaa kwenda kwenye mfuko wa mikopo ya vikundi na kusimamia urejeshwaji mikopo iliyotolewa miaka ya nyuma," alisema.

Alisema katika mwaka wa fedha 2024/25, serikali imepanga kutoa mikopo ya Sh. bilioni 228 ambapo kati ya hizo, Sh. bilioni 63.7 ni fedha za marejesho zilizokuwa zikiendelea kukusanywa kutokana na mikopo iliyotolewa kabla ya kusimamishwa Aprili mwaka jana.

Alisema Sh. bilioni 63.2 ni fedha zilizokuwa zinatengwa kwa ajili ya mikopo na Sh. bilioni 101.1 ni fedha ambazo zimetengwa kutokana na makisio ya makusanyo ya mapato ya ndani ya mwaka 2024/25.

Majaliwa alisema serikali imepanga utaratibu wa kutumia benki kwa halmashauri 10 za majaribio ambazo ni Majiji ya Dar es Salaam na Dodoma, Manispaa za Kigoma Ujiji na Songea, Miji ya Newala na Mbulu, Wilaya za Siha, Nkasi, Itilima na Bumbuli.


Jinsi Ya Kununua Magazeti Ya Nipashe na The Guardian katika tovuti ya www.ippmedia.com au epaper.ippmedia.com

Kupitia tovuti ya epaper.ippmedia.com:

1. Utafungua tovuti ya epaper.ippmedia.com utachagua toleo unalotaka kununua aidha Nipashe au The Guardian kwa kuclick Read
2. Itakuletea ukurasa mwingine unaotakiwa kujaza taarifa zako na kifurushi unachotaka kujiunga. Kisha unabonyeza "subscribe"
3. Itakupeleka katika ukurasa wa malipo ambapo unaweza kulipa kwa kadi ya benki malipo kwa mtandao wa simu unaoutumia baada ya kujaza kwa usahihi taarifa zako na anuani
4. Kwa namba ya simu unachagua mtandao wa simu unatumia ambapo utaandika namba yako na kutick box la kukubali terms and conditions. Itakuletea maelekezo kwenye simu yako namna ya kulipa ambapo utaweka namba ya siri na kuruhusu muamala. Malipo yakikamilika, utapokea email na message kuwa pesa imepokelewa hivyo utaingia kwa account yako na kuanza kusoma yale matoleo umeyalipia
5. Kwa benki unaweka taarifa za kadi yako ndio uruhusu muamala ukatwe katika account yako baada ya kukubali terms and conditions. Ndipo utaingia katika account yako na kusoma toleo ulilolilipia

Na kwa tovuti ya www.ippmedia.com

6. Unafungua website yako ya www.ippmedia.com upande wa kulia utaona "E-Paper" utabonyea na kuafuatisha hatua zote 1-5



For more Information Contact 0677 020 701 | Subscription: 0625 174 714 | Email: customerrelations@guardian.co.tz

Nipashe The Guardian

# Mbowe atamba CHADEMA inachukua uongozi wa nchi

**Na Godfrey Mushi,** BABATI

MWENYEKITI wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Freeman Mbowe, amesema Chama Cha Mapinduzi (CCM) "hakitatoboa" katika Uchaguzi Mkuu mwakani.

Akizungumza jana na wananchi wa Dareda, Wilaya ya Babati, mkoani Manyara, Mbowe alisema, "Ninawahakikishia mwaka ujao (wakati wa Uchaguzi Mkuu) ndio mwisho wa CCM. Uchaguzi huru na wa haki hawawezi kutoboa.

"Tunatafuta tena nguvu tuinyanyue CHADEMA kule ilikokuwa, iweze kuwa sauti ya wananchi. Uchaguzi wa vijiji na mitaa mwaka huu, Kata nzima ya Dareda na kata jirani, tukawafundishe CCM kwamba wameshaishiwa nguvu, hawana uwezo wa kushinda. Sisi tutashinda kwa mapenzi ya wananchi, kwa sababu Mungu yuko upande wa wale wanaoitafuta haki.

"Tunasema angalao tupite kata kwa kata kadri iwezekanavyo, tuwasalimie wananchi tuwatie moyo, msikate tamaa mambo mazuri yanakuja."

Mbowe alisema wanakwenda kushindana na CCM huku akiwaaminisha wananchi kwamba mwaka ujao kuna uwezekano mkubwa kuwa ndiyo mwisho wa CCM kuongoza nchi. Akiwa Dareda, Mbowe aliwataka wakazi wa eneo hilo kuhakikisha wanarejesha wabunge na madiwani wa CHADEMA.

**ULEVI KWA VIJANA**

Mwenyekiti wa CHADEMA Kanda ya Kaskazini na Mbunge wa zamani wa Arusha, Godbless Lema, akiwa Haydom, Dongobesh, Katesh na Dareda, alisisitiza kwamba hivi sasa kuna tatizo la ulevi wa kupindukia linaloitesa nchi.

Lema alisema tatizo hilo limesababisha vijana wadogo wenye umri kati ya miaka 20 na 40 kuwa wagonjwa wa figo.

"Leo vijana wadogo ndio wagonjwa wa figo ambao ni kati ya miaka 20 na 40. Hii ni kwa sababu ya pombe kali. Umasikini umewafanya wakapoteza matumaini, wakawa walevi, wanakula dawa za kulevya.

"Tunaongea kwa ajili ya watoto hawa kwa kuwa watakuja kuyachapa fimbo makaburi yetu kwa kushindwa kuona nchi inaharibika. Watu leo ni masikini, hali mbaya, vijana wote wameishia kuwa madereva bodaboda, hakuna viwanda, hakuna mashamba, hakuna uchumi. "Dada zetu wanakwenda mjini kuwa '... (alitaja neno lenye maana ya biashara haramu), hali ni mbaya, wote hapa mmevaa mitumba, mnajitia moyo, huo ni umasikini. Tunaagiza chumvi nje ya nchi kati ya Sh. bilioni 20 hadi Sh. bilioni 30 wakati Bashnet kuna chumvi," alisema.

Lema alishauri serikali kufikiria kufungua kiwanda cha chumvi Bashnet ili kuzuia chumvi ya nje ya nchi kuingia kwa kuwa kufanya hivyo katika Mkoa wa Manyara kutatoa ajira kwa wananchi wake.

Kuhusu mchele, Lema alisema mchele wa Magugu ni bora duniani, lakini unaishia Arusha na Dar es Salaam.

"Ukichukua mchele wa Magugu leo ukaupeleka Marekani, kilogramu moja ni Dola nane, Dola 10. Dola 10 ya Marekani, ni karibu 25,000 ya Tanzania. "Maana yake gunia la kilogramu 100 utauza Marekani milioni 2.5. Serikali ingeenda kwa wakulima wa Magugu, ingewaambia chukueni mitaji hii, lima mashamba laki moja (100,000), laki mbil (200,000i, laki tatu (300,000).

"Weka kiwanda cha kupaki mchele, weka track (malori) ya kupeleka mchele Arusha, weka kwenye treni peleka Tanga-Bandarini, peleka Marekani.

"Mchele ambao mpaka umetoka shambani umetumia Sh. 1,000 kwa kilogramu. Vijana wote wangeajiriwa na kujiajiri mashambani, wangepewa mikopo na wangelipa bima ya afya kwa wote na familia zao 'zingekula bata'," alisema Lema huku akishangiliwa na wananchi.



Watuhumiwa wa mauaji ya mtoto mwenye ualbino, Asimwe Novath (2) akiwemo Padre wa kanisa katoliki Jimbo la Bukoba Elipidius Rwegoshora, wakiwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Mfawidhi Mkoa wa Kagera jana, kabla ya kusomewa shtaka la kuua kwa kukusudia. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Tisa wapandishwa kizimbani kwa shtaka kumuua Asimwe

**Na Restuta Damian,** KAGERA

WATU tisa wamefikishwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Mfawidhi Mkoa wa Kagera kwa tuhuma za mauaji ya mtoto mwenye ualbino, Asimwe Novath (2).

Asimwe aliuawa na kukatwa viungo vyake vya mwili na kisha mwili wake kutelekezwa katika kalavati wilayani Muleba, mkoani Kagera.

Washtakiwa hao walifikishwa jana mahakamani huko ikiwa ni takribani mwezi mmoja tangu kuripotiwa tukio hilo Mei 30 mwaka huu katika Kata ya Kamachumu, wilayani Muleba.

Washtakiwa katika kesi hiyo ni Padri wa Kanisa Katoliki Jimbo la Bukoba, Elipidius Rwegoshora na Novart Venant, ambaye ni baba mzazi wa mtoto Asimwe.

Wengine ni Ramadhani Selestine, Nurdin Masoud, Rwenyagira Burukadi, Dunstan Burchard, Faswiu Athman, Gozbert Alchard na Dezdery Evergist ambao walisomewa shtaka moja la mauaji ya kukusudia.

Walisomewa shtaka hilo na Mwendesha Mashtaka Mkuu wa Serikali Mkoa wa Kagera, Waziri Magumbo, aliyesaidiwa na Wakili Mkuu wa Serikali, Erick Mabagala, mbele ya Hakimu wa Mahakama ya Hakimu Mkazi Bukoba, Elipokea Yona Wilson.

Magumbo alidai kuwa uchunguzi wa shauri hilo namba 17740 la mwaka 2024 umekamilika. Hakimu Wilson aliahirisha shauri hilo hadi Julai 12 mwaka huu kwa ajili ya kutajwa.

Washtakiwa walirejeshwa rumande kwa kuwa mahakama hiyo haina uwezo kisheria kusikiliza kesi hiyo.

Mei 30 mwaka huu, mtoto Asimwe aliripotiwa kuporwa kwa mama yake mzazi na watu wasiojulikana waliodaiwa kutokomea naye.

Juni 17 mwaka huu, mwili wa mtoto huyo ulikuwa katika kalavati, huku Jeshi la Polisi likieleza kuwa baadhi ya viungo vyake vilikuwa vimenyofolewa.

# TIRA kutumia Sabasaba kutoa elimu Bima ya Afya kwa Wote

**Na Restuta James**

MAMLAKA ya Bima Tanzania (TIRA) imepanga kutumia Maonesho ya 48 ya Kimataifa ya Biashara, maarufu Sabasaba, kuelimisha wananchi kuhusu Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote.

Pia imejipanga kutoa elimu kuhusu umuhimu wa kukata bima ili ifikapo mwaka 2030, asilimia 80 ya Watanzania wawe na uelewa wa huduma hizo.

Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa TIRA, Zakaria Muyengi aliyasema hayo jijini Dar es Salaam jana wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu huduma za bima zitakazopatikana wakati wa maonesho ya Sabasaba mwaka huu.

Alisema mamlaka hiyo ina wataalamu wa bima mbalimbali pamoja na wadau wake ambazo ni kampuni 40 zinazotoa huduma hizo ambao wamejipanga kuelimisha wananchi.

"Tunataka tuongeze uelewa na umuhimu wa bima kwa Watanzania kutoka asilimia 20 hadi 25 ya wenye bima sasa hadi asilimia 50 mwaka 2030," alifafanua Muyengi.

Kaimu Mkurugenzi huyo aliomba wananchi kujitokeza kupata elimu hiyo na kwamba wenye migogoro au madai kwa kampuni za bima watahudumiwa pia.

"Msuluhishi wa migogoro ya bima yupo hapa, mwananchi yeyote mwenye tatizo aje amwone ili shida yake itatuliwe," alisema.

Ofisa Mtendaji wa Muungano wa Kampuni za Bima, Elia Kajiba, alisema wananchi wenye madai mbalimbali watapatiwa huduma wakati wote wa maonesho.

"Bima ni rafiki wa jamii kuanzia afya, makazi, kilimo, biashara na maisha kwa ujumla kwa sababu inakukinga dhidi ya majanga mbalimbali.

"Tunawaalika wananchi wa Dar es Salaam na mikoa jirani waje wapate huduma, hata wale wenye madai hapa ni mahali sahihi kuja," alisema.

"Una madai yako unafuatilia, hapa ni mahala sahihi pa kupata mrejesho. Kama una mgogoro na kampuni yoyote, hapa ni sehemu sahihi kabisa," alisema Kajiba.

Serikali imekusudia kutumia mapato yatokanayo na pombe kali, vinywaji baridi, vipodozi na kamari, kuhudumia Bima ya Afya kwa Wote kupitia Sheria ya Fedha ya Mwaka 2024.

# HESLB yatangaza msako wa wadaiwa sugu mikopo yake

**Na Pilly Kigome**

BODI ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB) imezindua kampeni maalum ya kusaka wadaiwa sugu 50,000 ambao ni wanufaika wa mikopo ili kukusanya Sh. bilioni 200.

Akizungumza na waandishi wa habari jana jijini Dar es Salaam, Mkurugenzi Mtendaji wa HESLB, Dk. Bill Kiwia, alisema kampeni hiyo waliyoipa jina la 'FICHUA KUWA HERO WA MADOGO', ilianza rasmi jana.

Dk. Kiwia alisema lengo la kampeni hiyo ni kuhamasisha Watanzania kushirikiana na HESLB kufichua wadaiwa sugu walioko ofisini, nyumbani, mitaani na kwingineko, ili fedha hizo zikusanywe na kusaidia wengine wenye uhitaji.

Alisema kampeni hiyo itasaidia na kuchochea zaidi kuongeza uwezo wa kutoa mikopo na kuongeza kiwango cha mikopo.

Dk. Kiwia alisema wadaiwa hao watawapata kwa kutumia wanafunzi, watu mashuhuri, mitandao ya kijamii, vyombo vya habari, kampuni simu na wananchi wazalendo ambao wana uchungu na maendeleo ya elimu nchini.

"Lengo ni kufichua wadaiwa sugu ambao wana vipato, lakini wako mitaani wanaendelea na shughuli zao na hawashtuki kulipa madeni.

"Tunashukuru kuna baadhi ya wananchi wazalendo walikuwa wakitutumia majina ya watu wao wa karibu na tunawafuatilia, alisema Dk. Kiwia.

Akizungumzia hali ya urejeshaji mikopo, Mkurugenzi wa Urejeshaji na Urejeshwaji Mikopo HESLB, George Mziray, alisema ni nzuri na wamekuwa wakikusanya wastani wa Sh. bilioni 15 kwa mwezi kutoka kwa wanufaika 220,000 ambao wameajiriwa na kujiajiri.

Alisema endapo watawafikia wadaiwa wote, kiasi cha fedha kitakachokusanywa kitakuwa ni Sh. bilioni 200.

Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa alisema bungeni jijini Dodoma jana kuwa HESLB imeendelea kukusanya mikopo iliyoiva kutoka kwa wanufaika wa mikopo.

"Kwa mwaka 2023/24, serikali ilipanga kukusanya Sh. bilioni 230 ambapo hadi kufikia Mei 2024, Sh. bilioni 161 zilikusanywa sawa na asilimia 70 ya lengo," alisema.

Majaliwa pia alisema kuwa kwa mwaka 2024/25, serikali imetenga Sh. bilioni 787 kwa ajili ya kukopesha wanafunzi 250,000, wakiwamo 80,000 wa shahada ya kwanza ambao ni wapya.

"Maandalizi ya awali yameanza ikiwa ni pamoja na kusambaza mwongozo wa upangaji na utoaji mikopo; kufungua dirisha la uombaji mikopo kwa mwaka 2024/25 kwa muda wa siku 90 kuanzia Juni Mosi hadi 31 Agosti 2024; na kutoa elimu kwa waombaji mkopo na wadau wengine," alisema.

Majaliwa alisema kuwa kwa mwaka wa fedha 2023/24, serikali ilitoa mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu 224,056 na hadi kufikia Juni mwaka huu, wanafunzi hao walikuwa wamepatiwa mikopo yenye thamani ya Sh. bilioni 743.2 sawa na asilimia 94.6 ya fedha zilizotengwa.

Mikopo hiyo ilitengwa kwa ajili ya wanafunzi wa ngazi ya stashahada, shahada ya awali, stashahada ya juu ya mafunzo ya sheria kwa vitendo, shahada za umahiri na uzamivu, na ufadhili wa Samia (Samia Scholarships) katika masomo ya sayansi, teknolojia, uhandisi na hisabati.

Wanafunzi mnufaika Khadija Sultani anayesomea Shahada ya Usimamizi wa Biashara katika Chuo cha Kikuu cha Tumaini na Japhet Makyao anayechukua Shahada ya Udaktari na Upasuaji katika Chuo Kikuu cha Kimataifa Kampala, wameomba Watanzania kurejesha mikopo hiyo ili wenzao wengine wanufaike.

Wawili hao walisema jana katika ofisi za HESLB jijini Dar es Salaam kwamba kupitia bodi hiyo wameweza kutimiza ndoto zao kielimu kwa kuwa wasingemudu gharama kutokana na kufiwa na wazazi wao.



Askofu Mkuu wa Jimbo Kuu la Kanisa Katoliki Dar es Salaam, Mhashamu Yuda Thadei Ruwaichi (katikati), akizungumza wakati wa hafla ya chakula cha jioni kilichoandaliwa na Agape Center kwa ajili ya kuchangia ujenzi wa Kituo cha Mafunzo ya Kiroho na Stadi za Jamii, jijini Dar es Salaam juzi. Wengine ni Askofu Msaidizi wa Jimbo hilo, Mhashamu Stephano Musomba (kushoto) na Mhashamu Askofu, Henry Mchamungu. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# 20,000 watibiwa Kliniki ya Makonda

**Na Beatrice Shayo,** ARUSHA

ZAIDI ya wagonjwa 20,000 wametibiwa kwa siku nne katika kambi ya matibabu inayoendelea mkoani Arusha, huku wengine wakipatiwa rufani kwa ajili uchunguzi zaidi katika hospitali mbalimbali nchini.

Vilevile, viongozi wa dini wamejitokeza katika kambi hiyo ya matibabu na kuwaombea dua wananchi hao.

Hayo yamo katika taarifa ya Mkuu wa Mkoa wa Arusha, Paul Makonda aliyoitoa jana wakati akizungumza na wananchi waliojitokeza katika kambi hiyo ya matibabu bila malipo kwenye Uwanja wa Sheikh Amri Abeid, jijini.

Alisema idadi hiyo ya waliotibiwa ni kubwa, akiwataja hao ni wananchi waliokuwa wanaishi nyumbani wakiwa wamekata tamaa, hawana fedha ya kumwona daktari, kununua dawa na kufanya vipimo.

"Walijikatia tamaa na kumwomba Mungu wao, bahati nzuri amewasikia kilio chao na ndio maana tunashukuru kwa idadi hiyo kubwa na watu wamezidi kuongezeka, tayari tumeongeza idadi ya madaktari na dawa," alisema Makonda.

Alisema tayari wameunda kamati ya rufani na kuna wanaopimwa na kupatiwa dawa na wengine wanapelekwa hospitali nyingine kwa ajili ya upasuaji. "Ombi langu, tuwe na uvumilivu, ukiambiwa uende Hospitali ya Mount Meru si kwamba ukifika tu unafanyiwa upasuaji, zipo taratibu za kufanyiwa upasuaji, si kwamba ukifika tu unaanza kusema nimeambiwa nikifika ninafanyiwa upasuaji... fuata taratibu, hakuna ambaye ataachwa bila kupatiwa matibabu," alisema Makonda.

Alisema lengo lao ni kuhakikisha kila mmoja anapatiwa matibabu na kurejea katika afya yake, hivyo ni muhimu kwa kila mmoja kufuata maelekezo wanayopatiwa.

"Ukifika hospitalini na kuanza kusema nimeambiwa nifanyiwa upasuaji, eti Mkuu wa Mkoa kasema leo hii, si sawa! Suala la afya halina amri. Pamoja na ukuu wangu wa mkoa ninatii maelekezo ya daktari, ninaomba tusikilize maelekezo tunayopatiwa," alisema.

Makonda alisema dawa za kisukari, shinikizo la dawa na za masikio alijulishwa ziliisha, lakini hivi sasa zimepatikana, kila mwananchi mwenye shida kiafya atapatiwa.

"Dawa zote zimepatikana, usiondoke bila kupatiwa dawa. Tayari kuna wadau wetu wa Heko Phamacy Ltd wametupatia msaada za dawa ambazo zilikuwa zimeisha zenye thamani ya Sh. milioni 56," alisema Makonda.

Mkuu wa Mkoa huyo aliomba viongozi wa dini wafike katika kambi hiyo kuwaombea wananchi hao kwa kuwa anaamini katika Mungu.

"Nimewaomba viongozi wangu wa dini watufanyie dua ili Mwenyezi Mungu atupatie wepesi kwenye dawa tunazozitumia na madaktari watupatie dawa sahihi tukapate kupona," alisema Makonda.

Askofu wa KKKT Dayosisi ya Kaskazini Kati, Godson Mollel, alisema wanashukuru kwa kazi kubwa anayoifanya Makonda kwa namna alivyogusa maisha ya wananchi.

"Ninamshukuru na Rais Samia Suluhu Hassan kwa upendo wake katika mkoa huu na mikoa mingine kwa kuunga mkono jitihada za afya zinazoendelea, tunamshukuru Mungu kwa viongozi wetu kuonesha moyo wao wa kuwasaidia," alisema.

Askofu huyo pia alisema Makonda alianza na wiki ya haki na hivi sasa yuko kwenye afya, kukiwa na umati wa watu waliojitokeza kupokea huduma. Inajirihidhisha wana uhitaji mkubwa, lakini wanakosa fursa za kupata huduma hizo.

Alitoa wito kwa viongozi wengine nchini kuwa na moyo wa kusaidia wananchi huo, akiutaja ndio uongozi wanaohitaji.

"Makonda ameonesha mfano na wengine wafanye hivyo, hasa wanavyotazama huu umati wa watu na huduma hii inavyoendelea katika uwanja huu. Tunajua Mungu anaponya na vifaa hivi na wataalamu wetu Mungu atabariki matibabu hayo na Watanzania watapona, kilichotokea ni fursa ya matibabu," alisema.

Sheikh wa Mkoa wa Arusha, Shaaban Abdallah, alisema jambo lililofanywa linatakiwa kuungwa mkono na kila mmoja kwa sababu linachochea upendo miongoni mwa wananchi.

"Jambo hili lina manufaa makubwa, tunamwomba Mungu aendelee kumpa nguvu na ubunifu na mambo mengine yaliyo na manufaa na maslahi kwetu wananchi.

"Tunamwomba Mwenyezi Mungu jambo hili lilete tija nzuri na madaktari wetu Mwenyezi Mungu aendelee kuwapa nguvu na kuwaonesha cha kufanya kwa ajili ya magonjwa yetu na dawa zote zitakazotolewa zikapate baraka ziweze kuwaondolea watu wetu matatizo waliyokuwa nayo," alisema.

Mfamasia kutoka Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Arusha (Mount Meru), Frank Sanko, alisema walipatiwa dawa za kutosha, changamoto iliyojitokeza ni wingi wa watu, hivyo wanahitaji kuongezewa nguvu katika dawa.

Alisema kuongezwa dawa kutasaidia wananchi kuondoka wakiwa wamepatiwa matibabu kamili ikiwamo kupata dawa wanazozihitaji.

Baadhi ya wananchi wameomba waongezwe muda wa kutibiwa katiba kambi hiyo kwa kuwa siku zilizopangwa (saba) ni chache na bado kuna foleni kubwa.

Mkazi wa Arusha, Sarah Mtoba, alimwomba Makonda kuongeza siku za matibabu kutokana na wingi wa wananchi waliojitokeza kuhitaji huduma hiyo.

"Uhitaji ni mkubwa, foleni imeendelea kuwa ndefu, tunamwomba Makonda atusaidie kuongeza siku za matibabu na atuongezee madaktari ili kuhakikisha kila mmoja anahudumiwa," alisema Mtoba.

Meneja wa Tawi la Heko Phamacy Ltd ya mkoani Arusha, Sankirth Tekalkote, alisema wameguswa kuchangia huduma kwa wananchi hao ili wapate dawa.

# MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## Klabu Ligi Kuu Bara kumiliki timu za wanawake iwe sheria

**WAKATI** msimu wa Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania ulimalizika kwa Simba Queens ya Dar es Salaam kutwaa ubingwa bila kupoteza mechi hata moja, pazia la Ligi ya Mabingwa wa Mikoa (WRCL), lilifungwa rasmi jana.

Ligi hiyo iliyokuwa inachezwa jijini Dodoma inatoa timu mbili zinazopanda daraja kwenda Ligi Daraja la Kwanza kwa Wanawake (WFDL) katika msimu ujao wa mwaka 2024/2025.

Simba Queens sasa amepata tiketi ya kuiwakilisha Tanzania Bara katika mashindano ya kimataifa ya Klabu Bingwa Afrika Mashariki na Kati kwa Wanawake (CECAFA), yatakayofanyika baadaye mwaka huu.

Ili wawakilishi hao wafanye vizuri, wanahitaji kuwa wametoka katika ligi yenye ushindani na iliyoshirikisha idadi kubwa ya timu na si bingwa ambaye amebeba taji kwa kucheza na timu dhaifu.

Ukomavu wa mwakilishi wa nchi hupelekea kwenda katika mashindano ya kimataifa akiwa na kiwango bora na hapo haendi kwenye michuano hiyo kama msindikizaji, jambo ambalo halitakiwi kutokea.

Wakati tunalipongeza Shirikisho la Soka Tanzania (TFF) na Chama cha Mpira wa Miguu cha Wanawake Nchini (TWFA), kwa kusimamia na kuendesha vizuri Ligi za Wanawake na mashindano mengine mbalimbali, tunaliomba shirikisho hilo kuweka kanuni ya lazima kwa kila klabu ya Ligi Kuu Bara kumiliki timu ya wanawake.

Kwa kufanya hivyo, tutaongeza hamasa katika soka la wanawake kwa kuwa na idadi kubwa ya timu zitakazoshiriki Ligi Kuu kama ilivyo kwa upande wa wanaume.

Tunaamini kuwepo kwa kanuni hiyo inayolazimisha kuandaa kikosi cha wanawake, kutaendelea kutoa fursa kwa wachezaji wanawake lakini pia itawaongezea ajira wachezaji na wafanyakazi wengine wote watakaoajiriwa na klabu husika.

Wote tunafahamu michezo husaidia kuimarisha afya, hivyo timu za Ligi Kuu zinapomiliki klabu za wanawake kutawaongezea vipato kwa sababu baadhi ya mechi zimekuwa zinahudhuriwa ba idadi kubwa ya mashabiki ukilinganisha na wanapocheza wanaume.

Lakini sheria ya kuzitaka timu zote za Ligi Kuu zimiliki timu za wanawake zitasaidia hata pale klabu mojawapo itakapokata tiketi ya kushiriki mashindano ya kimataifa yanayoandaliwa na kusimamiwa na Shirikisho la Soka Afrika (CAF), haitaumiza kichwa kusaka timu ya 'kukodi' ili kutimiza sifa.

Tunashauri kuwepo kwa umiliki kwa sababu kuingia ubia au ushiriki, haifanyi klabu husika kushiriki kikamilifu katika shughuli za kila siku za uendeshaji tofauti na wanavyowajibika katika upande wa wanaume au timu za vijana.

Lakini kama ambavyo tunaamini wachezaji wazuri wa timu za taifa hupatikana kutokana na kuwapo kwa misingi mizuri ya soka la vijana, huu ni wakati wa TFF kuweka kanuni hiyo ambayo itasaidia kuongezeka kwa idadi kubwa ya wachezaji wanawake.

Itakuwa vigumu huko mbele kuziambia klabu zinazoshiriki Ligi Kuu Tanzania Bara kuwa na timu za vijana za wasichana za umri chini ya miaka 20 na U-17, wakati hazikuwekewa kanuni za kumiliki timu ya wanawake.

Mabadiliko ya kanuni yatasaidia zaidi kuzalisha wachezaji wanawake ambao waliotangulia wameonyesha uwezo mkubwa na kutangulia kushiriki fainali za Kombe la Dunia za umri chini ya miaka 17, wakati wanaume hawajawahi kukata tiketi ya kushiriki michuano yoyote inayoandaliwa na Shirikisho la Soka la Kimataifa (FIFA).

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Adam Fungamwango

### Wageni wanaosajiliwa wapimwe afya kuepuka wachezaji 'pancha'

**HIKI** ni kipindi cha usajili, huku timu zote zikisaka wachezaji kwa ajili ya kuboresha vikosi vyao.

Nimeona klabu nyingi za Ligi Kuu nchini zikisaka wachezaji kutoka nje ya nchi.

Hata Mashujaa FC nayo hivi karubuni, baadhi ya viongozi wao walikaririwa wakisema iwapo watapata ruhusu kutoka kwa mabosi wao Makao Makuu, wanaweza kusajili wachezaji wa kigeni.

Ikumbukwe kuwa Mashujaa ni timu inayomilikiwa na Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ), hivyo kwa taratibu zao hairuhusiwi kuwa na wachezaji kutoka nje ya nchi, labda kama kibali kitatolewa, tusubiri tuone.

Kwanza kabisa nipende kuzipongeza klabu nyingi za Tanzania ambapo kwa miaka ya hivi karibuni wamekuwa wakileta wachezaji wenye uwezo mkubwa na kuiheshimisha ligi yetu. Ligi ya Tanzania Bara kwa sasa inahesabika kuwa ni moja kati ya ligi bora barani Afrika, ikikamata nafasi ya sita.

Imekuwa ikileta wachezaji ambao kila mwaka wanamezewa mate na klabu kubwa na tajiri barani Afrika. Zamani huwezi kukutaeti mchezaji hata wa Simba au Yanga anatakiwa na klabu ya Mamelodi Sundowns, Kaizer Chiefs za Afrika Kusini, au Al Ahly na Zamalek za Misri, ila kwa sasa tunaliona hilo likitokea.

Luis Miquissone, winga raia wa Msumbiji ni mfano wa hili, alisajiliwa na Al Ahly akitokea Simba.

Fiston Mayele, mshambuliaji raia wa Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo, alisajiliwa na klabu ya Pyramids ya Misri akitokea Yanga.

Cha kufurahisha, hata klabu kama za Singida Big Stars, Tabora United na Coastal Union kwa miaka ya hivi karibuni zimekuwa zikisajili wachezaji wa kigeni wenye uwezo mkubwa kiasi cha kutamaniwa hata na klabu kubwa za Simba, Yanga na Azam FC.

Pamoja na hayo yote kuna kitu bado naona hakijakaa sawa na kama kikiwekwa vizuri Ligi ya Tanzania inaweza kuwa ndiyo bora zaidi Afrika.

Kuna baadhi ya wachezaji kutoka nje wanasajiliwa wakiwa na majeraha sugu na kuzipa hasara klabu, pamoja na ligi yenyewe.

Kama nafasi za hawa magonjwa zingechukuliwa na wachezaji waliofiti ingawezekana kabisa ligi ingekuwa ya kuvutia zaidi.

Simba, Yanga na Azam, ambazo zinasajili wachezaji wote 12 wa kigeni wanaoruhusiwa kwa kiasi kikubwa si wote wanaokuwa fiti kwa asilimia 100.

Wengine wanatoka huko walikotoka wakiwa na majeraha ya kudumu, kiasi kwamba wanapofika kwenye klabu hizi wanazifanya kama wodi za wagonjwa, huku wakiwa wanapokea mishahara. Mfano mdogo tu Simba ilimsajili Aubin Kramo mwanzoni mwa msimu uliopita, lakini hadi leo hawajafaidi matunda yake. Alicheza mechi moja tu ya Simba Day dhidi ya Power Dynamos, baada ya hapo hakucheza tena kwa kile kilichodaiwa kuwa na majeruhi.

Ukiangalia kwa umakini utagundua kuwa siyo majeraha ambayo aliyapatia Simba bali alitoka nayo huko, ila alikuja nchini na kujitonesha.

Azam FC imekuwa mara kwa mara ikilazimika kuwasafirisha wachezaji wake nchini Afrika Kusini kwa matibabu.

Wengi wao ni majeraha ambayo wametoka nayo huko, hii yote ni ukosefu wa umakini katika kuwapima afya.

Wakati wenzetu nje huko wako makini kuwapima kwa manufaa ya mchezaji mwenyewe na klabu, huku inafanywa kama fasheni tu, sijui huwa wanapima nini.

Sijawahi kusikia mchezaji hakufuzu vipimo, ila huko Ulaya wachezaji kadhaa wanafeli vipimo, huku klabu inaogopa kumpoteza mchezaji. Matokeo zinakuwa na wachezaji 'pancha' ambao wanakula tu pesa ya klabu bila kuzalisha chochote. Hivyo nashauri kuelekea Ligi Kuu msimu ujao, klabu zifanye vipimo vya ukweli ili kuondokana na kusajili wachezaji wenye majeruhi wa kudumu.

Ni bora kuwa na wachezaji pungufu ya 12, kuliko kuwa na wafanyakazi hewa kutokana tu na kushindwa kufuatilia historia zao, pamoja na kutowafanyia vipimo kamilifu.

VIFO WATOTO WATATU

## Watumishi wasimamishwa kazi kupisha uchunguzi

**Na Godfrey Mushi, ARUSHA**

WATUMISHI wawili wa Kituo cha Afya Levolosi, jijini Arusha, wamesimamishwa kazi kupisha uchunguzi wa tuhuma za kushindwa kutekeleza majukumu yao na kusababisha watoto watatu wa familia moja kupoteza maisha katika ajali ya moto iliyotokea Juni 22, mwaka huu.

Uamuzi huo umefikiwa baada ya kupokea taarifa kutoka katika mitandao ya kijamii Juni 23, mwaka huu, mwananchi akilalamika kucheleweshwa kupatiwa huduma kwa wagonjwa watatu wa ajali hiyo waliofikishwa katika kituo hicho siku ya tukio.

Taarifa iliyotolewa juzi na Mkurugenzi wa Jiji la Arusha, Juma Hamsini, ilieleza kuwa watumishi hao wanapisha uchunguzi wa tuhuma zinazowakabili za kushindwa kutekeleza majukumu yao.

"Waliosimamishwa kupisha uchunguzi ni Fatma Amir (mtumishi aliyekuwa eneo la mapokezi) na Kamwana David (Ofisa Tabibu aliyetoa huduma ya matibabu)," alisema mkurugenzi huyo katika taarifa hiyo.

Hamsini alisema timu ya kufuatilia tuhuma hizo tayari imeshaundwa na ripoti itawasilishwa kwa mwajiri.

Mkurugenzi huyo pia ametoa maelekezo kwa watumishi wote wa umma kuzingatia weledi na maadili ya utumishi wa umma wanapotoa huduma kwa wananchi.

Juni 22, mwaka huu, watu wanne wa familia moja, wakazi wa Mtaa wa Olmatejoo, jijini Arusha, walipoteza maisha akiwamo askari wa daraja la kwanza wa Shirika la Hifadhi za Taifa (TANAPA) anayefanya kazi Hifadhi ya Taifa ya Serengeti, baada ya makazi yao kuteketea kwa moto.

Kwa mujibu wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, chanzo cha moto huo ni kompyuta mpakato (laptop) iliyokuwa imechomekwa katika soketi ya umeme, kushika moto na kuunguza kochi.

Mbali na kusababisha vifo pia, moto huo pia ulijeruhi watu wengine saba, akiwamo mtoto mchanga wa siku nne, ambao walikimbizwa Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Arusha (Mount Meru).

Waliopoteza maisha ni baba mzazi wa watoto hao, Zuberi Msemo, aliyefariki dunia wakati akipatiwa matibabu hospitalini huko na watoto wake; Mariam Zuberi (9), Salma Zuberi (7) na Bisma Zuberi (3).

Majeruhi wanaoendelea na matibabu katika Hospitali ya Mount Meru ni mama wa watoto hao, Jasmine Khatibu (33), Mariam Mussa (60), ambaye ni mama mzazi wa Zuberi na Mwanaid Aldina (50), Mussa Msemo (34), AbdulKarim Ramadhan (9) na mfanyakazi wa ndani aliyefahamika kwa jina moja la Easther (20).




Mkurugenzi wa Tafiti za Mazingira wa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), Dk. Menan Jangu akionyesha jarida linaloelezea madhara ya zebaki, wakati alipozungumza na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam jana. Kulia ni Mratibu wa Mradi wa Kudhibiti Zebaki, Dk. Betrina Igulu. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# NEMC yataka teknolojia za kisasa uchenjuaji madini

**Na Joseph Mwendapole**

BARAZA la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) limesema limefanikiwa kuwezesha maabara nne kubwa nchini kupata teknolojia ya kisasa ya kuchenjua dhahabu ambazo zitawezesha wachimbaji wadogo kuachana na matumizi ya zebaki.

Mratibu wa Mradi wa Kudhibiti Zebaki wa NEMC, Dk. Betrina Igulu, aliyasema hayo jana wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu mafanikio ya mkakati wa kitaifa kupunguza matumizi ya zebaki.

Alisema teknolojia hiyo ya kisasa ndiyo inatumiwa na mataifa mbalimbali kwenye kuchenjua dhahabu na lengo la kuziwezesha maabara hizo ni kuachana na matumizi ya zebaki ambayo imekuwa na madhara makubwa ya kiafya kwa wanaoitumia.

Dk. Igulu alisema maabara zilizowezeshwa kuwa na teknolojia ya kisasa ni pamoja na Maabara ya Tume ya Madini, Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali, Maabara ya Taasisi ya Jiologia na Utafiti wa Madini (GST) na maabara ya NEMC.

Alisema mkakati wa kitaifa wa kupambana na matumizi ya zebaki umesaidia maelfu ya wachimbaji wa dhahabu kutambua matumizi salama ya zebaki na wengine kuachana nayo na kuamua kutumia teknolojia ya kisasa.

Alisema wachimbaji wengi wadogo wamekuwa wakipendelea zaidi matumizi ya zebaki katika kuchenjua dhahabu kutokana na urahisi wake wa kutumia na ni gharama nafuu zaidi.

Mratibu huyo alisema katika kutoa elimu kuhusu madhara ya matumizi ya zebaki, wamekuwa wakishirikiana na wadau mbalimbali, wakifanikiwa kuwafikia maelfu ya wachimbaji dhahabu mikoa mbalimbali.

"Tunasisitiza matumizi salama ya zebaki, kupunguza matumizi yake na ikiwezekana wachimbaji wadogo wa dhahabu waachane kabisa na njia hii, watumie njia za teknolojia ya kisasa ili kupunguza madhara yanayopatikana kwa binadamu," alisema.

Mratibu huyo alisema NEMC, Wizara ya Afya, Ofisi ya Mkemia Mkuu wa Serikali wamekuwa wakifanya tathmini ya kuangalia maeneo ambayo wameshindwa kutimiza wajibu wao na kusababisha wananchi kuendelea kutumia zebaki.

Alisema serikali na taasisi zake hizo imekuwa ikifanya marekebisho ya sheria na miongozo mbalimbali ili kuhakikisha inasimamia ipasavyo matumizi ya zebaki na haiendelei kusababisha madhara kwa wananchi wanaoitumia.

Alisema zebaki imekuwa ikipunguza uwezo wa kinga mwili, hivyo kuwa katika hatari ya kupata magonjwa kama saratani na mengine ambayo husababisha ulemavu wa kudumu.

Alisema wamekuwa wakiwafundisha wachimbaji wadogo matumizi sahihi ya zebaki na namna ya kuwa na teknolojia mbadala na kuwawezesha wachimbaji kuzitumia.

"Ukitumia zebaki kuchenjua dhahabu unaweza kupata asilimia 30 tu ya dhahabu wakati ukitumia teknolojia zingine za kisasa unaweza kupata hadi asilimia 90.

"Wachimbaji wadogo wanapenda zebaki kwa sababu ya urahisi wa upatikanaji wake, lakini tunaendelea kuwaelimisha kuhusu madhara," alisema.

Alisema teknolojia ya za kisasa zimekuwa zinatumiwa na wachimbaji wakubwa kutokana na gharama zake kuwashinda wachimbaji wadogo wa dhahabu katika mikoa mbalimbali.

Alisema kwa kuliona hilo, NEMC iliweka mikakati kuhakikisha zinapatikana teknolojia mbalimbali kwa gharama ndogo ili wachimbaji wengi wapate na kuitumia na kuachana na matumizi ya zebaki kuchenjua dhahabu.

Mkurugenzi wa Utafiti wa Mazingira NEMC, Dk. Menan Jangu, alisema lengo la baraza ni kuhakikisha wachimbaji wanakuwa salama wakati wote wanapokuwa katika uchimbaji wa madini.

Alisema sekta ya madini inachangia fedha nyingi katika Pato la Taifa, lakini upatikanaji wake umekuwa na athari kubwa katika mazingira kuanzia uchimbaji na uchakataji wake, hasa wanapotumia zebaki.

"Lengo letu ni hizi shughuli zifanyike kwa namna ambayo haiathiri mazingira nchini. Inakadiriwa kuwa kuna wachimbaji wadogo milioni 1.5. Sasa wakifanya kazi zao katika mazingira hatarish, Watanzania wengi wataathirika.

"Ndiyo maana Tanzania kwa kushirikiana na Global Fund na Benki ya Dunia (WB) ikaja na mradi wa kukabiliana na matumizi ya zebaki kwa wachimbaji katika mikoa saba nchini.

"Wachimbaji wengi wanaona ni rahisi kuitumia zebaki kulinganisha na teknolojia zingine, lakini madhara yake ni magonjwa kama saratani, mtindio wa ubongo, uzazi na mengine mengi," alionya mkurugenzi huyo.



Wajumbe wa Bodi ya Shirika la Nyumba nchini (NHC), wakikagua majengo mbalimbali yanayojengwa na shirika hilo katika mradi wa Samia Housing Scheme Kawe, Manispaa ya Kinondoni, Dar es Salaam juzi. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Wamwangukia Samia machimbo yao kupewa mwekezaji mkubwa

**Na Mwandishi Wetu, aliyekuwa** SONGWE

WACHIMBAJI wadogo wa madini wapatao 300 katika Kijiji cha Kampilipili, Kata ya Mbangala, wilayani Songwe, wamemwomba Rais Samia Suluhu Hassan kuingilia kati mgogoro ulioibuka baada ya kuondolewa machimbo eneo hilo.

Wakizungumza na waandishi wa habari hivi karibuni, wachimbaji hao walisema kuwa tangu mwaka 2011 wamekuwa wakichimba madini katika eneo hilo kwa ajili ya kujipatia kipato cha kuendeshea maisha na familia zao bila usumbufu.

Mwenyekiti wa Wachimbaji hao, Goodluck Mungure, alisema katika hali ya kushangaza, hivi karibuni wataalamu kutoka ofisi ya madini wakiongozwa na Ofisa Madini Mkazi wa Mkoa wa Songwe, Chone Malembo walikwenda kutambulishwa ujio wa mwekezaji katika eneo hilo.

Malembo alisema jambo hilo limewashangaza kwa kuwa kwa miaka 13 wako katika eneo hilo wakichimba madini na kufuata taratibu na sheria kama serikali inavyotaka.

Wachimbaji hao waliendelea kulalamika kuwa walishangazwa kupewa taarifa kuwa eneo hilo amepewa mwekezaji ambaye hata hivyo hawajawahi kumwona na hajawahi kufika katika kijiji hicho.

Walisema kitendo cha kuwaambia waondoke eneo hilo kwa kuwa kapewa mwekezaji kimewashtua kwa kuwa hawajawahi kushirikishwa tangu mwanzo mchakato wa kupatiwa. Walisema hawapingani na uamuzi wa serikali kutafuta mwekezaji mwingine katika eneo hilo, lakini kabla ya kufanya hivyo, wangeshirikishwa wachimbaji ambao wamekuwapo kwa muda mrefu badala ya kuwashtukiza na kuwaamuru waondoke wakati wawekeza fedha zao.

Walisema kuondolewa ghafla katika eneo hilo bila kutafutiwa njia mbadala maana yake ni kuwaangamiza kiuchumi wakati serikali inatambua wachimbaji wadogo wa madini ambao ni nguzo muhimu katika kukuza uchumi kupitia sekta ya madini.

Kwa mujibu wa wachimbaji hao, kuna wasiwasi kwamba kuna jambo limejificha nyuma ya pazia kwa ajili ya kulinda maslahi binafsi.

"Tumekopa mikopo katika taasisi za fedha kwa ajili kununua vifaa vya uchimbaji vinavyolingana na uwezo wetu, sasa leo hii tunapoambiwa tuondoke ili apewe mwekezaji mwenye fedha zake, huu ni unyanyasaji wakati na sisi ni Watanzania na tuna haki ya kufaidi matunda ya rasilimali za nchi hii," walilalama.

Mwenyekiti wa Wachimbaji Wadogo Mkoa wa Songwe, Kamaka, alisema wanapinga uamuzi wa kumpa mwekezaji apewe eneo hilo ambalo wachimbaji hao wamekuwapo kwa muda mrefu.

Kamaka alisema serikali inapaswa kuingilia kati haraka suala hilo kunusuru uvunjifu wa amani eneo hilo hasa katika kipindi hiki cha mchakato wa Uchaguzi wa Serikali za Mitaa.

Malembo alipoulizwa na Nipashe kuhusu malalamiko hayo, alithibitisha kuwapo mgogoro baada ya kwenda kumtambulisha mwekezaji katika eneo hilo.

Mkuu wa Wilaya ya Songwe, Solomoni Itunda aameagiza kusimamisha shughuli zote za uchimbaji katika eneo hilo kwa sababu za kiusalama.

"Ninakuagiza Ofisa Madini Mkoa shughulikia suala hili kwa kushirikisha pande zote ili kupata suluhu," alisema.

Juni 20 mwaka huu, Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango, aliagiza Wizara ya Madini na Tume ya Madini kusimamia wachimbaji wadogo waliopata leseni kuwekeza kwenye mitaji yao ili wasinyang'anywe maeneo kwa kisingizio walipewa kwenye maeneo ya wachimbaji wakubwa.

Akizungumza jijini Dodoma wakati wa ufunguzi wa Maonesho ya Wiki ya Madini 2024 yaliyoandaliwa na Shirikisho la Vyama vya Wachimbaji Madini Tanzania (FEMATA), alisema amepokea malalamiko kadhaa kuhusu hilo la kutoondolewa mchimbaji mdogo katika eneo la uchimbaji kwa ajili ya kuwapisha wawekezaji wa madini wakubwa.

Dk. Mpango alisema serikali imeendelea kutenga maeneo kwa ajili ya wachimbaji wadogo na kurasimisha maeneo yenye milipuko wa madini.

# Majaliwa ahimiza utekelezaji mkakati nishati safi ya kupikia

**Na Robert Hokororo,** DODOMA

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa amehimiza wadau wote kushiriki kikamilifu katika utekelezaji Mkakati wa Taifa wa Matumizi ya Nishati Safi ya Kupikia (2024-2034) ili kufikia malengo ya utunzaji mazingira.

Alitoa rai hiyo kauli hiyo wakati akitoa hoja ya kuahirisha Mkutano wa 15 wa Bunge jijini Dodoma jana, akisisitiza kuwa matumizi ya nishati safi mbali ya kuimarisha utunzaji mazingira pia yataboresha afya na ustawi wa jamii.

"Mheshimiwa Spika, nitoe wito kwa wizara za kisekta, taasisi, idara za serikali, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, asasi za kiraia, sekta binafsi, wadau wa maendeleo, wabunge na Watanzania wote kushiriki katika utekelezaji mkakati huu," alisema.

Waziri Mkuu alisema kampeni ya matumizi ya nishati safi ya kupikia inaendelea kote nchini na tayari maelekezo thabiti yameshatolewa na Ofisi ya Makamu wa Rais.

Aliongeza kuwa miongozo iliyotolewa inaendelea kusimamiwa kikamilifu sanjari na utoaji elimu ili wananchi wapate uelewa na hivyo kuachana na matumizi ya nishati chafu ambayo yanachangia ukataji miti kwa lengo la kupata kuni na mkaa. Inakadiriwa kuwa takribani hekta 469,000 za misitu hupotea kila mwaka wakati nishati za kuni na mkaa zikitajwa kuwa ni chanzo kikuu cha kutoweka kwa misitu hiyo.

Itakumbukwa kuwa mkakati huo ulizinduliwa na Rais Samia Suluhu Hassan tarehe 8 Mei mwaka huu, ukitoa mwongozo wa kitaifa kwa wadau wote kuhakikisha nchi inafikia lengo lililojiwekea la asilimia 80 ya Watanzania kutumia nishati safi ya kupikia ifikapo mwaka 2034.

Lengo la mkakati huo likitekelezwa na kutimia, litapunguza gharama ya nishati safi ya kupikia pamoja na kuongeza upatikanaji na uwekezaji nishati hiyo.

Bunge limeahirishwa hadi tarehe 27 Agosti mwaka huu. Katika mkutano huo wa 15, chombo hicho kilipitisha Bajeti ya Serikali ya Sh. trilioni 49.35 kwa mwaka wa fedha 2024/25 ambayo pamoja na mambo mbalimbali pia inaakisi sekta ya mazingira.

# NHC kuanzisha mkoa wa kiutendaji Urafiki

**Na Joseph Mwendapole**

KATIKA jitihada za kuimarisha ufanisi na kuchochea maendeleo katika eneo la Urafiki, wilayani Ubungo, Dar es Salaam, Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) limepanga kuanzisha mkoa mpya wa kiutendaji Urafiki.

Hatua hiyo ilitangazwa jana na Mkurugenzi Mkuu wa NHC, Hamad Abdallah, wakati akitoa taarifa kwa Bodi ya Wakurugenzi wa shirika hilo inayofanya ziara katika miradi mbalimbali kufahamu hatua za utekelezaji na changamoto.

Alisema mkoa huo mpya wa kiutendaji unalenga kuongeza uratibu bora wa shughuli za maendeleo na huduma kwa jamii katika eneo la Urafiki.

Alisema lengo la kuanzisha mkoa huo ni kuwezesha utoaji huduma bora za makazi na miundombinu muhimu kwa wakazi wa eneo hilo na kukuza fursa za kiuchumi na kijamii.

Mkurugenzi huyo alisema Urafiki ni moja kati ya maeneo yenye ukuaji wa haraka mkoani Dar es Salaam na kuanzishwa kwa mkoa mpya wa kiutendaji kunatarajiwa kuongeza usimamizi thabiti na ufanisi katika utoaji huduma za maendeleo ya jamii na miundombinu ya makazi.

"Mpango huu unakusudia pia kuleta mabadiliko chanya katika maisha ya wakazi wa Urafiki kwa kuimarisha mifumo ya utawala na usimamizi.

"Hatua hii inaonesha dhamira ya NHC katika kuhakikisha maendeleo endelevu na ustawi wa jamii katika eneo la Urafiki, na inatarajiwa kuleta manufaa makubwa kwa wenyeji wa eneo hilo na jamii kwa ujumla," alisema.

Akitoa taarifa kuhusu eneo la Urafiki, Mkurugenzi wa Usimamizi Miliki, Elias Msese, alisema lina jumla ya Units 399, majengo sita ya biashara, makazi 32 ya wataalamu, shule ya msingi, maduka ya rejareja 32, maghala 31, yard za magari 10, gereji nne, kituo cha mafuta kimoja, sehemu tatu za kuosha magari, 'Industrial park', flemu ndogo na kontena.

Alisema kwa kuanzia, shirika linaweza kukusanya Sh. bilioni moja kwa mwezi na kiasi hicho kitaongezeka kadri maboresho yanavyofanyika.

Mwenyekiti wa Bodi ya NHC, Dk. Sophia Kongela alipongeza hatua zote muhimu zilizopigwa baada ya makabidhiano na kutaka shirika kuweka mipango ya haraka ili kuliboresha eneo hilo.

Dk. Kongela aliwataka wajenzi wa miradi hiyo kuhakikisha inakuwa na ubora unaotakiwa na inakamilika kwa wakati.

"Ni muhimu kwa bodi yetu kufanya ziara kama hizi ili kujionea moja kwa moja maendeleo ya miradi yetu. Tunajivunia juhudi zinazofanywa na timu yetu ya ujenzi na lazima tuhakikishe miradi yote inatekelezwa kwa viwango vya kimataifa," alisema Dk. Kongela.

Bodi ya Wakurugenzi ya Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) imezuru katika miradi mbalimbali ya shirika hilo iliyoko Dar es Salaam kwa lengo la kukagua maendeleo ya ujenzi.

Katika ziara hiyo, bodi ilipata fursa ya kutembelea miradi ya Kawe 711, Morocco Square, Samia Housing na eneo la NHC Urafiki ambayo inajumuisha ujenzi wa nyumba za makazi na biashara.

Bodi inaendelea na ziara katika miradi ya Samia, Morocco Square na Eneo la NHC Urafiki kufuatilia utekelezaji wa maelekezo na miongozo yake.



## EWURA yapiga marufuku uuzaji mafuta kwenye vidumu

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

MAMLAKA ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) Kanda ya Kati umewataka watu wanaouza mafuta kwenye vidumu kuacha mara moja ili kunusuru maisha yao.

Meneja wa EWURA wa Kanda hiyo, Hawa Lweno alibanisha hayo jana jijini hapa wakati akizungumza na waandishi wa habari wakati wa kikao cha wadau wa sekta ya nishati na maji.

Lweno, alisema tabia ya watu kuuza mafuta kiholela kwenye vidumu ni hatari kwa maisha yao kwa kuwa maeneo wanayoyatumia siyo salama.

"Uuzaji wa mafuta kwenye vidumu na maeneo yasiyo rasmi unaweza kusababisha majanga ambayo yatagharimu maisha ya watu wengi, hivyo nitoe wito kwa Watanzania wenzangu kuacha tabia hii ni hatari sana kwetu na kwa wale wanaotuzunguka,"alisema

Meneja Mawasiliano na Uhusiano EWURA, Titus Kaguo, alisema lengo la kikao hicho na wadau hao ni kutoa elimu kuhusu huduma wanazozitoa.

Kaguo, alisema moja kati ya changamoto iliyopo ni ukosefu wa elimu kwa jamii kuhusu huduma zinazotolewa na mamlaka hiyo.

"Changamoto ambayo imejitokeza zaidi katika kikao hiki ni pamoja na usomaji mita za maji na upatikanaji wa mkataba wa huduma kwa wateja," alisema.

Alisema katika changamoto ya usomaji mita, watu wengi hawajui gharama halisi za uniti za maji hali ambayo imekuwa ikiibua malalamiko ya kubambikiziwa ankara za malipo.

"Pia watu bado hawajui umuhimu wa mkataba wa huduma kwa wateja ambao wanaweza kupata katika mamlaka husika na kuwasaidia kujua haki zao kwa huduma wanazozistahili," alisema Kaguo.

Alitaja moja ya majukumu ya mamlaka hiyo ni kulinda mitaji ya wawekezaji na walaji kwa kudhibiti ubora wa bidhaa wanazozizalisha.

"Jukumu mojawapo la EWURA ni kulinda mitaji ya wawekezaji kama mwekezaji atashindwa kupata faida na kufunga uwekezaji basi itakuwa imeshindwa kutekeleza wajibu wake wa kusaidia kulinda mtaji wa mwekezaji,"alisema

Alilitaja jukumu jingine kuwa ni kuchochea uchumi na maendeleo kwa kuhakikisha bidhaa zinazohakikiwa na mamlaka hiyo zinakuwa na ubora.

"Kama tukipima mafuta basi ubora ule hata mtu akitoka nje ya nchi akiweka mafuta yake kwenye gari liwake, lakini hata maji tunayazalisha hapa yawe kwenye ubora uleule na mataifa mengine yaliyoendelea," alisema.

Mwenyekiti wa Umoja wa Wajasiriamali Tanzania, Issa Njoka, alisema moja kati ya changamoto wanazokutana nazo katika uzalishaji wa bidhaa zao ni ukosefu wa umeme wa uhakika.

Njoka, alisema hali hiyo imekuwa ikisababisha kuzalisha bidhaa zisizokuwa na ubora kutokana na kukosekana kwa umeme wa uhakika.

# Wanawake hawa hatarini kupata kifafa cha mimba

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

WANAWAKE wenye umri zaidi ya miaka 35 wako hatarini kupata ugonjwa wa kifafa cha mimba kwa kuwa na uhusiano wa kimapenzi na zaidi ya mwanaume mmoja.

Kauli hiyo ilitolewa juzi na Mtaalam wa Magonjwa ya Wanawake Hospitali ya Rufani Kanda ya Benjamini Mkapa (BMH), Dk. Christopher Mzimya wakati akizungumza na waandishi wa habari jijini hapa.

Akizungumza wakati wa mafunzo kwa wataalamu wa afya kubaini mapema watu wenye ugonjwa huo, Dk. Mzimya, alisema dalili za kifafa cha mimba huanza kipindi cha wiki ya 20 kwa mwenye ujauzito.

Alizitaja dalili za awali kuwa ni kuwa na shinikizo la damu na kukutwa na protini kwenye mkojo.

Alisema dalili mbaya zaidi za ugonjwa huo ni shinikizo la damu kuwa juu na kupungua kupata mkojo na hiyo inaashiria figo kuathirika.

"Mgonjwa anapokuwa na shinikizo la juu la damu kuanzia 160 kwenda juu na mkojo kupungua hadi 30 mls kwa saa, mgonjwa huyu anasemekana kuwa na hali mbaya na anaweza kupata kifafa cha mimba," alisisitiza.

Dk. Mziya, alisema mwanamke anaweza kupata ugonjwa huo endapo atakuwa na mahusiano na wanaume tofauti tofauti na kuwa na umri mkubwa.

"Endapo mwanamke atakuwa na mahusiano na wanaume tofauti, kuwa na umri zaidi ya miaka 35 na kuwa na uzito mkubwa ana hatihati ya kupata preeclampsia," alisema

Alisema njia za kujikinga na ugonjwa wa huo, kabla ya kubeba ujauzito mwanamke anatakiwa kufanya vipimo ili kujua kama ana shinikizo la damu, kisukari na wenye umri mkubwa kutumia dozi ndogo ya aspirini na ya calcium.

Mkurugenzi wa Utawala na Rasilimaliwatu BMH, Prisca Lwangili alipendekeza elimu hiyo kuwafikia watu wengi katika jamii kupitia vyombo vya habari na maandiko ili kuondokana na dhana potofu katika jamii.



Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk. Doto Biteko (kushoto), akijadiliana jambo na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu, Jenista Mhagama (katikati) na Waziri wa Fedha, Dk. Mwigulu Nchemba, Bungeni jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Wanasiasa wanaochafua viongozi kukiona

**Na Thobias Mwanakatwe,** ITIGI

MKUU wa Mkoa wa Singida, Halima Dendego amewaonya wanasiasa na mtu anayeingia mkoani humo na kuanza kukashifu na kutukana viongozi wa juu wa Serikali atakamatwa na kuchukuliwa hatua.

Dendego ambaye pia ni Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama, alitoa onyo hilo juzi kwenye mkutano wa hadhara uliofanyika uwanja wa stendi ya Itigi kwa ajili kusikiliza kero zinazowakabili wakazi wa Halmashauri ya Itigi na kuzitafutia ufumbuzi.

Alisisitiza kuwa hatakubali kusikia wala kuona viongozi wakuu wa Serikali wakitukanwa na kudhalilishwa mkoani kwake wakati yeye yupo, hivyo watakaothubutu kufanya hivyo, watakiona cha moto. Alisema wakazi wa Singida ni watu wa amani na wanataka maendeleo, ikiwemo ya barabara, maji, shule, afya na mbolea na si matusi na kwamba anayetaka kuvunja amani na utulivu watashughulika naye.

"Vijana wa Mkoa wa Singida acheni kukaa kimya viongozi wanapotukanwa bali muwajibu kikamilifu kupitia mitandao ya kijamii kuhusu kazi kubwa inayofanywa na Serikali katika kuwaletea wananchi maendeleo," alisema.

Dendego, aliwataka wakazi hao wa Singida kwa umoja wao kuwakataa wanasiasa wanaotaka kuwagawa wananchi kwa udini, ukabila au rangi kwa sababu Watanzania wote ni wamoja tangu enzi na wanashirikiana katika masuala ya kijamii.

Alisema vyama vya siasa vilianzishwa nchini vishindane kwa hoja na sio matusi kwenye majukwaa.

Mkuu huyo wa mkoa, aliendele kusema wananchi wakiona baadhi ya vyama vinafanya hivyo, basi wajue kuwa havina sera na hakuna sababu kwenda kwenye mikutano yao.

Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Singida, Martha Mlata, akizungumza kwenye mkutano huo, aliwataka wakazi hao kuwapuuza wanasiasa wanaofika kwenye maeneo yao na kufanya siasa za uhasama na uchochezi.

Mlata aliwahimiza kuendelea kuunga mkono jitihada za Serikali ya Awamu ya Sita kwa kuwa imeonyesha dhamira ya dhati kuwaletea maendeleo katika sekta za afya, elimu, maji na miundombinu.



# Mwinyi ataka wananchi wauziwe gesi bei nafuu

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

RAIS wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ), Dk Hussein Ali Mwinyi amezitaka kampuni za gesi kuwawezesha wananchi kununua nishati hiyo kwa bei nafuu ili waachane na matumizi ya kuni na mkaa majumbani.

Dk.Mwinyi alitoa rai hiyo wakati akizindua bohari ya kwanza ya kuhifadhia gesi ya Kampuni ya Oryx Gas Zanzibar Limited iliyopo Mangapwani, Mkoa wa Kaskazini Unguja.

Alisema ametoa rai hiyo wananchi waondokane na matumizi ya mkaa ili kupunguza athari uchafuzi, uharibifu wa mazingira na hewa sumu.

Alipongeza kampuni hiyo kwa kujenga matangi mawili yenye ujazo wa tani 1,388 sawa na kilo 1,388,000 za gesi.

Alisema matumizi ya nishati zisizo salama hasa mkaa na kuni zinazochochea ongezeko la athari za mabadiliko ya tabianchi na magonjwa yatokanayo na kuvuta hewa yenye sumu.

Alisema kwamba matumizi ya makaa, kuni na ukataji hovyo wa miti, kwa kiasi kikubwa kunachangia uzalishaji wa hewa ya kaboni, ambayo imekuwa ikisababisha athari mbalimbali.

Dk. Mwinyi alisema bohari hiyo itakayohifadhi gesi Zanzibar itakuwa chachu ya utekelezaji wa mpango wa matumizi ya nishati safi ya kupikia wa mwaka 2024/34 uliozinduliwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. Samia Suluhu Hassan.

Aliipongeza wizara na Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar (ZURA) kwa usimamizi wa sekta ya gesi visiwani hapa na kampuni hiyo kwa uwekezaji huo mkubwa.

Kwa mujibu wa Dk. Mwinyi, kwa miaka mingi, uingizaji wa gesi nchini umekuwa ukifanyika kupitia Bandari ya Malindi na kampuni nne.

Oryx Gas Zanzibar Limited, Lake Gas Tanzania Limited, Taifa Gas Tanzania Limited na O - Gas.

Alisema kutokana na ongezeko kubwa la shughuli za kiuchumi na kijamii, eneo hilo kwa sasa halitoshi kuendelea kutumika kwa gesi ikizingatiwa mazingira ya kiusalama kwa bidhaa hiyo.

Dk. Mwinyi, alisema kutokana na hali hiyo, serikali inatarajia eneo la Mangapwani kuwa bandari jumuishi itakayohusisha bandari ya mafuta na miundombinu ya kupokea na kuhifadhia nishati hiyo, gesi na bidhaa nyingine.

Alisema ujenzi wa miundombinu uko hatua za awali za kufanikisha lengo la kuwa na bandari ya kisasa ukanda wa pwani ya Afrika Mashariki.

Minyi, alisema serikali ilitenga eneo hilo kwa lengo la kuhakikisha usalama wa ugavi wa bidhaa za mafuta na gesi kwa kupokea meli kubwa zenye bidhaa ambazo zitaweza kukidhi mahitaji ya nchi kwa zaidi ya miezi mitatu bila.

Mkurugenzi Mkuu wa Oryx gas, Benoit Araman, alisema zaidi ya dola milioni 100 zimeekezwa katika kampuni hiyo na kutengeneza ajira za moja kwa moja na zisizo rasmi na kulipa kodi serikalini.

Araman, alisema mwanzoni mwa mwezi ujao, gesi itauzwa kwa bei nzuri na kusaidia utekelezaji wa matumizi nishati hiyo visiwa vya Zanzibar.

Mwenyekiti wa kundi la Makampuni ya Vigor, Taufik Turky, alisema kazi haikuwa rahisi kuhakikisha wanaweka bohari ya gesi Zanzibar.

Turky, alisema soko la gesi kwa Zanzibar ni tani 200 na mpaka wanaingia ubia na Oryx hivi umefikia tani 300.

Alisema utafiti unaonyesha kwa Zanzibar asilimia 12 ya wananchi wanatumia gesi na kuwahakikishia aliwahakikishia wananchi gharama hizo zitapunguzwa ili kila mmoja atumie nishati hiyo.

## 'Wanawake, watoto wapewe msaada wa sheria vijijini'

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MWENYEKITI wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar, Mwanaasha Khamis Juma, aitaka idara ya msaada wa kisheria kufikisha huduma vijijini kwa makundi ya jamii ikiwemo wanawake na watoto ili waondokane na changamoto katika ndoa na talaka.

Aliyasema hayo jana katika kongamano la malezi ikiwa ni sehemu ya Maadhimisho ya Wiki ya Msaada wa Sheria Zanzibar.

Mwenyekiti huyo, alisema katika jamii kuna changamoto zinawakabili wanawake kwa kukos msaada wa sheria kutokana na hali ngumu ya maisha.

Alizitaja baadhi ya changamoto hizo kuwa ni kupoteza haki za mirathi wanapofiwa na waume na kunyanganywa sehemu ya ardhi ambayo walitakiwa kurithi.

Alisema wanawake walikuwa wakipoteza haki katika umiliki wa ardhi wa eka tatu tatu zilizotolewa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ) kama warithi namba moja.

Aliitaka idara ya msaada wa kisheria kutoa huduma za kisheria kwa makundi ambayo yapo nyuma huku haki zao zikionekana kupuuzwa.

Vilevile, aliitaka taasisi hiyo kuleta mabadiliko ya sheria ambazo zinahitaji kufanyiwa kazi kwa lengo la kuleta ufanisi na kuondoa dhuluma na ukandamizwaji wa wanawake na watoto.

"Wito wangu sisi wawakilishi ndiyo tunaopitisha sheria zinazotungwa kama kuna sheria ambazo mnahisi zinahitaji kufanyiwa marekebisho zileteni sisi tutazifanyiya kazi mara moja," alisema.

Mkurugenzi wa Huduma za Msaada wa Kisheria wa SMZ, Hanifa Ramadhan Said, alisema wamejipanga huduma za msaada wa kisheria zinayafikiya makundi yote.

Kwa mujibu wa Hanifa, tangu kuanzishwa kwa idara hiyo takriban miaka sita, wanawake ndiyo wanaoonekana wenye mahitaji makubwa kwa kuwepo kwa changamoto kupata msaada wa sheria.

"Huduma zetu zinayalenga makundi yote, " alisema.




Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Othman Masoud Othman akizungumza wakati akifungua kongamano la tano la kitaifa la wafanyakazi na washiriki wa afya ya macho Tanzania, Mkoa wa Mjini Magharibi, juzi. **PICHA: MAELEZO - ZNZ**

# Wataalamu wa macho wapewa changamoto

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi amewataka wataalamu wa macho kutatua changamoto zinazoikabili jamii kwa ustawi na huduma bora za afya.

Akifungua Kongamano la Tano la Kitaifa la Chama cha Madaktari Bingwa wa Macho Tanzania (TOS) kwa niaba ya Dk. Mwinyi, Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Othman Masoud Othman, alisema kwa kufanya hivyo kutasaidia nchi zinazoendelea kuyafikia maendeleo endelevu.

Alisema SMZ kupitia Wizara ya Afya, itaendelea kushirikiana na chama hicho kuondoa baadhi ya changamoto zinazowakabili jambo na kuwawezesha wananchi kuendelea kupata huduma bora kutoka kwa wataalamu hao.

Dk. Mwinyi aliutaka uongozi wa chama hicho kutafuta uhusiano na mashirika mengine ya kimataifa ili kuwasaidia wanachama wao kuongeza ujuzi , uzoefu wa taaluma yao na kuleta mabadiliko chanya ya huduma za macho nchini.

Aliwapongeza wanachama wa TOS kwa kuandaa kambi ya macho kama sehemu ya maadhimisho ya mkutano huo jambo mbalo limesaidia wananchi waliojitokeza kupata matibabu haraka.

Waziri wa Afya Zanzibar, Nassor Ahmed Mazrui, aliwataka vijana kusomea taaluma ya matibabu ya macho ili kukidhi mahitaji kutokana na ongezeko kubwa la hospitali mpya za kisasa na wagonjwa wengi nchini.

Mazrui, alisema wizara hiyo inaendelea kuongeza wataalamu wa fani hiyo na kuwapatia mafunzo ya muda mrefu na mfupi kwa lengo la kutoa huduma bora kwa jamii.

Katibu Mkuu Wizara hiyo, Dk. Habiba Omar, alisema wataendelea kuwafikia wananchi wote wenye matatizo hayo ili kupunguza athari za uoni nchini.

Omar, alisema katika kipindi cha Januari hadi Disemba mwaka jana, zaidi ya watu 5000 walipatiwa huduma za macho katika kliniki za visiwa vya Unguja na Pemba. Akitoa salamu za chama hicho, Rais wake, Dk. Christopher Mwanansao, alisema kongamano hilo liliambatana na utoaji wa huduma kwa jamii.

Dk. Mwansao, alisema katika kongamano hilo lililoendeshwa na chama hicho katika kambi maalum ya siku nne, walifanikiwa kuchunguza zaidi ya watu 1,000. Alisema katika kipindi hicho, walifanya upasuaji kwa wagonjwa zaidi ya 160 ukiwemo wa kawaida na kisasa wa kutoa mtoto wa jicho kwa kutumia matundu madogo.

Alisema katika kambi hiyo, idadi kubwa ya wananchi waligundulika kusumbuliwa na presha ya macho na kusema ipo haja ya chama hicho kushirikiana na serikali kufanya utafiti zaidi juu ya tatizo hilo.

Alisema kuwa lengo la chama hicho ni kushirikiana na serikali katika kuimarisha huduma za macho, kufanya tafiti na kuwaunganisha wadau wa afya ya macho.



## SABI GIRL NI NANI?

UKURASA 14

Nipashe
MWANGA WA JAMII
BT
BURUDANI TELE
JUMAMOSI JUNI 29, 2024



# LIKO WAPI?

SWALI ambalo wengi wanauliza liko wapi lile penzi zito kati ya staa wa filamu za Bongo, Wema Sepetu na mwanamuziki Whozu?

Hata hivyo, hakuna mwenye jibu sahihi kama penzi la wasanii hao ambao walikuwa kila mara wakitawala katika mitandao ya kijamii kutokana na mahaba yao mazito, kama liko hai au la.

Wapo wanaoamini kwamba tayari Wema kaamua kuachana na Whozu kimyakimya, kutokana na sasa kujikita katika biashara zake pekee.

Hata katika ukurasa wake wa kijamii, Wema ameacha kuposti picha au video za Whozu kwa kipindi cha miezi minne mfululizo, jambo linaloashiria wawili hao wana shida.

Machi Mwaka huu, Wema alikaririwa akielezea afya yake kuwa iko vizuri baada ya taarifa ya kupokea kipigo kutoka mpenzi wake kusambaa.

Baadhi ya watu wanaofuatilia maisha ya wasanii, wamesema kinachoonekana sasa ni wazi hakuna mapenzi kati ya wawili hao, badala yake kila mmoja ameamua kunyamaza kimya akingalia maisha yake.

"Ninachokiona hakuna mapenzi, kilichobaki kila mmoja ameamua kukubali yaishe na waendelee na maisha mengine," amesema Yahaya Saidi.

Mara kwa mara taarifa zilizokuwa zikitoka ndani, zilieleza Wema alionekana kuchoshwa na tabia ya Whozu, ya kumpiga na kumfanyia ubabe.

BASI SAWA

## Koffi kuwapa raha kwa Mkapa



Mkongwe katika muziki wa dansi kutoka nchini Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, Koffi Olomide, ameahidi kuwapa burudani ya kipekee kwenye shoo yake atakayoifanya kesho katika uwanja wa Benjamini Mkapa, Dar es Salaam.

Akizungumza baada ya kutua nchini, Olomide, amesema amejiandaa kukutana na mashabiki wake na kitu atakachowapa kama zawadi ni kutoa burudani ambayo haijawahi kutokea.

"Natamani kukutana na mashabiki wangu kesho, nimefanya maandalizi ya kutosha ili watakapokuja uwanjani wapate burudani na hiyo ndiyo zawadi yangu ya kipekee kwao," amesema Olomide.

## Makabila hujifunzi tu



MSANII wa muziki wa Singeli, Dula Makabila, amemwagiwa sifa kutokana na kitendo chake cha kuomba radhi kutokana na kauli yake iliyomlenga Majizzo.

Makabila ambaye ana kawaida ya kutoa dukuduku lake hadharani, alimchafua bosi huyo wa EFM, akisema katika matamasha yake anayoyaandaa wanamuziki wa singeli wanawekwa nyuma.

Baadhi ya wafuasi wake waliousoma waraka wake wa kuomba radhi, wamemshauri msanii huyo kuacha kutoa tuhuma ambazo zinaweza kumuathiri kwani ni kawaida kwake kila wakati kuomba msamaha kwa matendo yake.



# RAYVANNY HAWEZEKANI TENA

INAWEZEKANA! Ndivyo staa wa muziki wa bongo fleva, Rayvanny, anavyotoa somo kwa wasanii wengine nchini baada ya kufanikiwa kujaza uwanja katika shoo yake aliyoifanya nchini Albania.

Tamasha hilo linaloitwa Noizy Alpha Show lililofanyika usiku wa kuamkia jana kulishuhudia jinsi watu walivyojaa katika uwanja, huku msanii huyo akielezea furaha yake kutokana na mafanikio hayo.

Rayvanny kwa sasa anaonekana kuweka nguvu kwa katika shoo zake za nje ya nchi ambazo zimeonekana kumletea mafanikio.



# Omondi alia akimuaga mdogo wake

MSANII wa uchekeshaji, Eric Omondi, amebubujika machozi wakati wa kuaga mwili wa mdogo wake, Fred Omondi, ambaye alifariki kwa ajali ya gari.

Katika moja ya video zilizosambaa mitandaoni, Omondi anaonekana akilia kwa huzuni huku mpenziwe Lynne na mchekeshaji mwenza, Terence Creative wakimfariji na kumshikilia.

Mwili wa Fred Omondi utasafirishwa hadi mji wa Siaya na mazishi yake yanafanyika leo.

Fred ambaye pia alikuwa mchekeshaji alifariki baada ya gari lake kupata ajali wiki mbili zilizopita.

FILAMU

# Mfalme Mwovu: Shikamoo mapenzi

**Na Adam Fungamwango**

MAPENZI ni kitu cha ajabu sana duniani. Ni kitu ambacho hata wanasayansi wameshindwa kukidadavua kwa usahihi, mtu akitaka kupenda au kupendwa afanye nini. Ni kitu kinachotokea tu ghafla bila sababu yoyote. Ndiyo kitu pekee duniani ambacho hakina tabaka la masikini au tajiri. Anayependa siku zote penye pengo huona mwanya na kwenye chongo kwake huwa ni kengeza tu.

Hapa leo tutaiangalia filamu ya 'Mfalme Mwovu' ambayo itatueleza kila kitu na kututhibitishia hili.

Baadhi ya wasanii waliocheza filamu hiyo ni mzee Msisiri wa Msisiri aliyecheza kama Mfalme Gotagota, Ally Sheria aliyecheza kama Mzengo, Khadija Rashid aliyecheza kama Anita na Hamdani Ibrahim aliyecheza kama Mgumo.

Kwenye himaya ya ardhi ya Nsangu anatokea kiumbe wa ajabu anayeishi porini. Kwa wananchi wa himaya hiyo kwao ni kiumbe wa ajabu, lakini ni binadamu wa kawaida kwa mwonekano, lakini anaishi porini akiwinda na kula wanyama. Ni kijana tu wa miaka 25, lakini kutokana na kujitenga na himaya hiyo pamoja na mavazi yake ya ajabu anaonekana ni kiumbe wa ajabu.

Msichana aliyekuwa akienda kuteka maji kisimani ndiye alimuona na kupeleka taarifa kijijini. Wakati anamkimbia, binti wa mfalme Anita alitaka kuanguka, lakini kijana huyo aitwaye Mzengo alimuokoa. Ikawa kosa. Binti mfalme akatokea tu kumpenda kijana huyo. Wasichana wenzake kijijini wakaanza kumcheka. Mfalme Gotagota akasikia hilo, akakasirika. Lengo ilikuwa ni kwamba Anita aolewe na askari mkuu Mguno.

Binti mfalme hamtaki Mguno, anamtaka Mzengo. Mipango inafanywa kwa mfalme na Mguno kumfanya aonekane mbaya.

Wanaua baadhi ya watu kwenye himaya na kusingiziwa kijana huyo. Anakamatwa na kutaka kuuawa na mfalme. Binti anapinga na kudai akiuawa na yeye anajiua. Mfalme anasitisha. Yanafanyika mashindano ya baiskeli kwenye himaya hiyo na atakayeshinda ndiye atamuoa binti mfalme. Mzengo anashinda kwa sababu alifundishwa kwa siri na binti mfalme. Mfalme anasalimu amri anampa mke kijana Mzengo. Kabla ya hapo anataka kujua alipotoka. Mzengo anaseme miaka mingi nyuma mama yake alifukuzwa kwenye kijiji hicho kwa tuhuma za uchawi wakati huo yeye akiwa mdogo. Akaenda kuishi porini hadi mama yake alipofariki na yeye kuishi peke yake hadi umri huo.




# WAR BUS, KOMANDO KIPENSI ENZI HIZO

**Na Adam Fungamwango**

MIAKA ya 1980, hadi katikati ya miaka ya 1990, kabla ya televisheni kuenea majumbani kuanzia katikati ya miaka ya 1990, vijana na watoto wengi walikuwa wakienda maeneo mbalimbali, ili kuona sinema.

Wengine walienda kwenye majumba makubwa ya sinema. Hao ni kwa wale kwenye uwezo. Wengine walikwenda maeneo ambayo yalikuwa yana afadhali kidogo. Lakini wengi wao hasa watoto walikuwa wakienda kwenye sehemu ambazo kwa sasa zinaitwa 'vibanda umiza'.

Huko utakuta mtu kazungushia tu magunia na ndani kaweka televisheni yake, akionyesha filamu mbalimbali.

Achilia mbali filamu za Kichina, ambazo nyingi ni za sanaa za mapigano, na kihindi ambazo tutakuja kuzizungumzia siku nyingine. leo tutaziangalia filamu za kizungu.

Kulikuwa na filamu nyingi maarufu za kizungu ambazo hakuna kijana au mtoto ambaye alitaka kuzikosa. Leo tunakwenda kuangalia filamu hizo.

**War Bus**

Ni filamu maarufu sana kwa Wabongo, ambayo ilitoka mwaka 1985. Mastaa wa picha hii ni Daniel Stephen, Romano Kristoff na Urs Althaus.

Msingi wa picha hii ni vita ya Vietnam. Ni makomandoo watatu wa Kimarekani waliokwenda kuwaokoa mateka walioshikiliwa na 'wavete', kama walivyokuwa wakiitwa watoto wakati huo.

Kilichovutia zaidi watazamaji wengi wa filamu hiyo, siyo operesheni hiyo, bali ni staili ya makomandoo hao ambao waliamua kuteka basi ya shule na kulitumia kama usafiri wa kwenda kuwaokolea watu wao. Ile staili ya ulinzi wa mmoja kukaa mbele ya boneti la basi, mwingine juu kwa ajili ya ulinzi, mwingine ndani, pamoja na mbwembwe zao, ndiyo msingi wa picha hii kupendwa.

**American Ninja**

Hii pia ni filamu ambayo iliwanyima watu usingizi, ilitoka mwaka 1985 kama 'War Bus'.

Wakubwa, vijana na watoto wa Kibongo waliipenda sana filamu hii, ikimhusisha staa mmoja anaitwa Michael Dudikoff. Huyu ni askari wa Kimarekani ambaye pia ana ujuzi mwingine wa kupigana na watu wanaitwa maninja, ujuzi alioupata akiwa mdogo.

Humu anatwangana na maninja kisawasawa na kuwshinda, kiasi cha kuwa moja ya filamu bora sana na kukumbukwa hadi leo.

**No retreat, no surrender**

Filamu hii ilitoka mwaka 1986. Hii siyo ya kivita kama 'War Bus'. Wala siyo ya mapanga na sanaa za kininja. Picha hili ni la sanaa wa mapigano. Humo ndani zimepigwa balaa. Stelingi kwenye filamu hii ni staa aliyekuwa maarufu sana wakati huo, Jean Claude van Damme. Huyu alisifika sana kwa mateke ambayo ndiyo yaliyokuwa yanampa zaidi ushindi. Ni moja kati ya filamu maarufu na iliyopendwa sana.

**Komando Kipensi**

Jina halisi ya picha hili ni 'Deadly Pray'. Lakini nadhani hadi leo si wengi wanaojua jina halisi ya filamu hii. Lakini ukiwaambia 'Komando kipensi', kila mtu atasema anaifahamu.

Sidhani kama kuna mtoto au kijana wa miaka ya 1980 mpaka 2000, ambaye haifahamu filamu hii. Ilitoka mwaka 1987.

Jamaa anaitwa Troy Donahue, au kwa jina la picha ni Mike Danton. Huyu ni jeshi la mtu mmoja. Anapigana akiwa amevaa pensi tu, ndiyo maana wakamwita hivyo. Alimchokoza wenyewe. Walikuwa hawajui kuwa ni mwanajeshi mstaafu. Walitaka kumfanya chambo. Ikawa ni vita vya ajabu.

**Delta Force**

Ilitoka mwaka 1986. Ni moja kati ya filamu maarufu sana kwa Wabongo wakati huo. Staa wa filamu hii ni mkongwe Chuck Norris. Ni picha la kivita.

# Huyu Sabi Girl ni nani?

MWANAMUZIKI wa Nigeria Ayra Starr, amefunguka kuhusu msemo wake wa 'Sabi Girl' akisema ni alama ya ujasiri na kujiamini.

Msanii huyo wakati akizungumza katika kipindi cha Touching Base kinachorushwa na MTV, katika ziara yake ya kutangaza albamu yake mpya inayoitwa 'The Year I turned 21,' ameeleza 'Sabi Girl' ni msemo wenye maana kubwa kwake.

"Sabi girl ni msemo ambao unamaanisha msichana mwenye kujiamini, mkarimu, na mwerevu. Lazima uwe na akili." Amesema.





## Mastaa wamlilia Bill Cobbs

WASANII mbalimbali duniani wanaendelea kuomboleza kifo cha mwigizaji mkongwe wa Hollywood, Bill Cobbs (90), ambaye alifariki Jumanne wiki hii.

Kulingana na mtandao wa TMZ, watu maarufu wakiwamo waigizaji wanaendelea kwenda nyumbani kwa Cobbs katika eneo la Inland Empire huko Calfonia, kutoa rambirambi zao.

Cobbs alikuwa na taaluma ya uigizaji iliyoanzia miaka ya 1970, na mpaka anafariki ametengeneza filamu 200 na maonyesho kadhaa ya televisheni.

Baadhi ya filamu alizoigiza wakati wa uhai wake ni Devaney, The Bodyguard, Louisiana Slim ya mwaka wa 1979 na The Brother from Another Planet.

## Mike aiwazia Grammy

MWANAMUZIKI wa Marekani, Killer Mike yuko katika hatihati ya kushiriki tuzo ya Grammy, baada ya kukabiliwa na matatizo ya kisheria.

Kulingana na mtandao wa TMZ. imegundulika kuwa msanii huyo kuwa hayuko sawa baada ya kukamatwa kwa kuhusisha ugomvi wake na mlinzi wake.

Waendesha mashtaka katika Ofisi ya Mwanasheria wa Jiji la Los Angeles, walisema kuwa hawatafungua mashtaka dhidi ya Mike kutokana na tukio hilo.





## Davido azindua ndege yake

MKALI wa muziki wa Afrobeat kutoka Nigeria, Davido Adeleke, amewashangaza mashabiki wake baada ya kutambulisha ndege yake mpya.

Davido ambaye amefunga ndoa hivi karubuni na mama wa watoto mapacha, Chioma, amenunua ndege hiyo kama zawadi kwa mkewe kwa ajili ya matembezi ya kifamilia.

Katika ukurasa wake wa X, Davido amewaambia wafuasi wake kuwa ndege hiyo ya kifahari itatumika kuwapeleka na kuwarudisha katika kufurahia fungate yao.

## Mzimu wa Mohbad bado unasumbua

BAADA ya mwaka mmoja tangu kifo cha mwanamuziki wa Nigeria, Mohbad, hatimaye mama wa msanii huyo ameibuka na kuomba uchunguzi mpya ili kubaini chanzo cha kifo chake.

Ilerioluwa Oladimeji Aloba, amesema mume wake ambaye ni baba mzazi wa msanii huyo hakubaliani na matokeo ya uchunguzi uliofanywa awali kutokana na kujaa utata.

Hata hivyo, ameeleza baba yake sasa ilitaka kufanyike vipimo vya DNA ifanyike kwa Liam, mtoto wa mwimbaji huyo ambaye wao hawamtambui.





HABARI KASKAZINI

# Migogoro yakwamisha 18 kulipwa fidia bomba la mafuta

**Na Oscar Assenga,** TANGA

WANANCHI 18 kati ya 1,580 walioathirika na mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP) linalotoka Hoima nchini Uganda hadi Chongoleani- Tanga, hawajalipwa fidia kutokana na sababu mbalimbali ikiwamo migogoro ya kifamilia.

Mratibu wa uhusiano ya jamii kutoka EACOP, Amanyile Mahali, alitoa taarifa hiyo jana, wakati wa semina ya wanahabari jijini Tanga, iliyokuwa na lengo la kuwapa uelewa kuhusu hatua za mradi na kuwajengea uwezo ili waweze kuwa na taarifa sahihi ambazo zinapaswa kuwafikia wananchi.

Alisema kwamba lakini asilimia 99 ya wananchi waliopisha ujenzi wa bomba hilo wameshalipwa fidia zao na waliobakia wanakamilisha taratibu zao wenyewe zikiwamo za kifamilia ili waweze nao kulipwa.

Mahali alisema kwamba sababu nyingine ambazo zimesababisha watu hao kutokulipwa fidia licha ya fedha zao kuwapo ni pamoja na watu wawili bado wanaendelea na michakato wa mirathi mahakamani, ambapo awali aliyeandikishwa alifariki duniani kabla ya kulipwa fidia na wakikamilisha watapata fidia yao.

Aidha, alisema pia watu wawili hawajulikani walipo na wanaendelea kutafutwa na watu 12 wana migogoro ya ardhi kama kifamilia wanaendelea kupelekana mahakamani pamoja na mmoja kukata kusaini mkataba kutokana na fedha aliyoipata hakutegemea.

Alisema kesi zote hazihusiani na bomba bali ni wao kwa wao, kwamba menejimenti wamewawekea fedha zao zipo tayari na utaratibu wao ukimalizika watapata fidia zao.

Alisema kwa makaburi Tanga Jiji, matano katika Mtaa wa Pande wameshayakamilisha kulipa fidia, Muheza makaburi ni mengi kidogo lakini zoezi la uhamishaji limeshakamilika.

Alisema kwa upande wa nyumba, Tanga zipo 11 za waathirika ambapo watatu waliotoka mitaa ya Kibafuta, Mabokweni zilijengwa Ndaoya Njia Panda kuelekea Chongoleani na nne zipo Mtaa wa Mleni na moja ipo Ndumbi, huku tatu zikiwa Pande.

Hata hivyo alisema kwa sasa wana programu katika mitaa ya Mabokweni, Chongoleani, Ndoaya ya kuboresha mazingira ya baharini ili kuwasaidia wavuvi watakuwepo kupitia (BMU), kwamba shughuli hizo walikuwa wanazifanya huko nyuma zitakuwa na ufadhili wa EACOP.

Awali, Mwenyekiti wa Chama cha Waandishi wa Habari, Mkoa wa Tanga, Lulu George, aliwashukuru EACOP kwa kutoa mafunzo kuhusu mradi wa mafuta ghafi.

Alisema mafunzo ya mradi huo ni fursa nzuri kwa kujengewa uwezo kuhusu shughuli za mradi kuanzia hatua za awali mpaka sasa zinazoendelea.

Alisema kwamba waandishi wa habari wamebeba jukumu kubwa la kwenda kuwaelimisha wananchi kuhusu fursa zilizopo na kuwashauri waandishi wa habari kuchukua mafunzo hayo kama fursa ya kwenda kuwaelimisha wanajamii.

Aidha, alisema kupitia mafunzo hayo yatawawezesha wanahabari kuwa na uelewa mpana wa kupata uzoefu mzuri ambao utawawezesha kwenda kuielimisha jamii zaidi kuhusu mradi huo.

Alisema: "Lakini waandishi wa habari hakikisheni mnapata taarifa kwa watu sahihi kuhusu taarifa za mradi huo na msiandike habari za kusikia za nje, badala yake muende kwenye vyombo vilivyokuwa na uhakika ambavyo vitaweza kutoa habari za kina".

Aidha, pia aliwataka kuandika habari kwa maslahi mapana ambayo yamejenga uzalendo ndani yake na kuhakikisha mradi huo unaweza kuimarika na kujivunia.

# Wajitosa kusaidia uhaba wa mashuka Hospitali ya Rufani

**Na Jaliwason Jasson,** MANYARA

JUKWAA la Vyama vya Ushirika mkoani Manyara, limejitosa kutatua tatizo la uhaba wa mashuka linaloikabili Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Manyara baada ya kutoa msaada wa mashuka 70 ili kuongeza ufanisi wa utoaji wa huduma kwa wagonjwa.

Akizungumza jana baada ya kutoa msaada huo, Mwenyekiti wa Jukwaa hilo, Yuda Sulley, alisema wameamua kutoa mashuka hayo kama sehemu ya huruma kwa wagonjwa.

Aidha alisema waliona wagonjwa wengi wanatoka kwa wanaushirika, hivyo wakaona ni vizuri kuwapa msaada huo ambao utaongeza ari ya utoaji huduma kwa madaktari na wauguzi.

Sulley alisema kila mwaka wanapofanya mkutano wa jukwaa wanatenga fungu maalumu la kuigusa jamii, hasa kwa watu wenye uhitaji ambapo mwaka jana walienda kuwapa msaada wazee wa Kituo cha Sarame kilichopo Kata ya Magugu wilayani Babati.

Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Mkoa wa Manyara, Dk. Catherine Magari, aliwashukuru wanaushirika hao kwa kuisaidia hospitali hiyo.

Dk.Magari alisema mashuka hayo yatawasaidia kwa kuwa vipo vitanda vilivyo kuongezewa mashuka, kwamba kila kitanda kinatakiwa kuwa mashuka nane ili mgonjwa awe anabadilishiwa kila siku.

Hivyo, aliahidi kuendelea kutoa ushirikiano kwa wanaushirika na jamii kwa ujumla ambayo inapata huduma hospitalini hapo.

Baadhi ya wagonjwa akiwemo Paul Simon alisema wanaushirika wamefanya jambo zuri kutoa msaada huo, akisema nao ipo siku wanaweza kutumia mashuka hayo wakiumwa.



Mratibu wa shirika la Mwambao coastal community Network Tanzania Mkoa wa Tanga, Ahmad Salim Omar (kulia), akikabidhi boti ya doria, kwa Katibu Tawala Wilaya ya Mkinga, Palango Abdul katika kijiji cha Boma Mahandakini juzi, kwa ajili ya kufanya doria kulinda rasilimali Bahari. **PICHA: BONIFACE GIDEON**

# CCM yaanza kuwapika vijana kuelekea uchaguzi

**Na Mary Mosha,** MOSHI

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM), kimeanza kutengeneza vijana maalum watakaobeba dhamana ya kutetea viti vyake vya wenyeviti wa serikali za mitaa 60 katika Manispaa ya Moshi, mkoani Kilimanjaro ili isiangukie mikono ya wapinzani.

Jana, Mwenyekiti wa Jumuiya ya Umoja wa Vijana Chama Cha Mapinduzi, Manispaa ya Moshi (UVCCM), Sadath Ndibalema, alisema vijana hao wamepewa mafunzo mbalimbali yakiwemo ya ukakamavu, uzalendo, kutetea chama hicho na kujitokeza kwa wingi kugombea nafasi mbalimbali kwenye uchaguzi huo.

Alisema vijana 300 walioibuliwa katika kila mitaa, waliwekwa kambini kwa siku tano kupigwa msasa wa namna watakavyokabiliana na hoja za wapinzani na kushinda uchaguzi ujao wa mitaa, vijiji na vitongoji, unaotarajiwa kufanyika Oktoba mwaka huu.

Ndibalema alisema kambi hiyo iliwekwa katika Chuo cha Maendeleo cha Singa, kilichopo Wilaya ya Moshi, mkoani kilimanjaro.

"Vijana hawa wamepata mafunzo ya aina nyingi ikiwemo kufundishwa uzalendo, kutetea chama chao na kusimamia misingi ya sheria, taratibu na kanuni za nchi katika kuelekea kwenye chaguzi, lengo ni kupata viongozi bora na wenye tija kwa jamii yetu watakaoleta tija,"alisema Ndibalema.

Akifunga mafunzo hayo, Mwenyekiti wa CCM, Mkoa wa Kilimanjaro, Patrick Boisafi, aliwataka vijana kuzingatia muda kwenye kila jambo, huku akisisitiza kutoridhishwa na taalumu zao.

"Vijana, punguzeni kupoteza muda kwa mambo yasiyo na tisha na kisha kujiita wasomi, ili uwe msomi mwenye tija ni lazima uweze kutafsiri ulichosoma kwa vitendo na kilete tija.

Vijana wengi mnalalamika hakuna ajira lakini nyinyi hamjitumi kuwa wabunifu katika kutatua matatizo ya jamii na pia wengi wenu siyo waaminifu, hii inafanya vijana kutoaminiwa kwenye kila eneo wanalofanya kazi hii siyo dalili nzuri kwa kizazi kijacho. Mnapaswa kujitathimini " alisema Boisafi.

Mwenyekiti wa UVCCM, Mkoa wa Kilimanjaro, Ivan Moshi, alisema kuwa watu ambao watakifanya chama kishinda kwa urahisi katika Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025 ni viongozi wa dola waliochaguliwa mwaka 2020.

Alisema kuwa baadhi ya madiwani wamekuwa hawafanyi mikutano ya hadhara ya wananchi lakini wamekuwa wakisuguana na wabunge, ambapo kila mmoja amekuwa akimtupia lawama mwenzake na kukiomba chama kuhakikisha kila kiongozi anatimiza wajibu wake.

Aidha, Mkuu wa Wilaya ya Moshi, Zephania Sumaye, alisema CCM kinahitaji vijana jeuri na wenye akili ya kuhoji jambo na kuweza kulitetea mbele ya jamii.

Sumaye alisema kesho ya Tanzania imewekwa katika mabega ya vijana na siyo rasilimali zilizopo ambapo kambi hizo zinasaidia vijana kupata elimu.

TULIKOTOKA, TULIPO & TUNAKOKWENDA

# Machinga vijana ‘ walivyoteka’ kazi ya wazee zamani kutembeza kapu la urembo

**Na Adam Fungamwango**

KABLA ya uhuru hadi miaka ya mwishoni mwa 1990, ilikuwa si ajabu kumuona mtu mzima akipita mitaani na kapu lililokuwa limejaa vipodozi vya akinamama kama vile bangili, hereni, rangi ya kucha, wanja, hina, vibanio vya nywele, vitana, chanuo, manukato na vitu vingine vinavyofanana na hivyo.

Wengine walipita kimya kwa wengine walikuwa wakipiga mbinja, yaani kutamka maneno ambayo yanayoashiria kuwa muuza vitu hivyo anapita.

Hii ilifanyika ili kama kuna mwanamama yupo ndani ambaye anahitaji chochote kati ya hicho, ajue muuzaji wa kitu anachotaka anapita.

Mwanadada au mama anayetaka kupaka rangi kwenye kucha atapakwa na mzee huyo, kama ni kipodozi chochote hata kama ni poda itanunuliwa hapo, na yeyote yule ambaye alikuwa anataka chochote atatoka ndani kuja kumuunga mkono mzee kwa atakachokinunua.

Baada ya hapo mzee atanyanyua kapu lake na kuanza kuita tena, “haya urembo urembo, muuza uzuri anapita...” Hivyo ndivyo walivyokuwa wanaitia.

Kwenye mikoa hasa ya Pwani hasa Dar es Salaam, Tanga, na Pwani yenyewe ilikuwa ndiyo biashara maarufu sana. Ila cha ajabu ilifanywa na watu wenye umri mkubwa, kama vile ilivyokuwa zamani kwa vinyozi, kazi iliyofanya na watu wazima chini ya miembe.

Kama ilivyokuwa kwa vinyozi ambao ‘wamepinduliwa’ na sasa biashara hiyo inafanywa na vijana, wakiifanya kisasa si chini ya miembe kwa kutumia viwembe na mkasi, bali kwenye maeneo ya biashara ndani ya vyumba ambavyo vina viyoyozi wakitumia mashine za kisasa, wateja wakikaa kwenye makochi badala ya kwenye viti vya mbao, watembeza uzuri nao yaliwakuta.

Maendeleo ya teknolojia yamekuja kuwaondoa wazee hao, kwani sasa hivi kazi hiyo inafanywa na vijana ambao ni maarufu kwa jina la wamachinga.

Achana na wale ambao wamekuwa wakipita na nguo, viatu na vingine, lakini wapo wanaopita na vipodozi, lakini wao hawaweki kwenye kapu la ukili kama wale mababu wa zamani. Kuna dizaini zao wenyewe, wabeba ‘kisharobaro’ na kupitisha mitaani.

Hii imekwenda mbali zaidi siku hizi kuna mpaka wakopeshaji. Nao ni vijana sana. Wanapita mitaani kukopesha nguo, khanga, vyombo vya ndani kama sufuria, mabeseni na kadhalika.

Hii inaonyesha kwamba kutokana na maendeleo ya uchumi na teknolojia, zile kazi ambazo wakati huo zilionekana ni za wazee, sasa hivi zinafanywa na vijana. Kwa haraka haraka unaweza kusema ni kutokana na ukosefu wa ajira. Inawezekana ingawa ni kwa asilimia fulani hivi, hili si la kupuuzwa hata kidogo, lakini utandawazi nao umechangia kwa kiasi kikubwa.





Picha zote zinaonyesha staili wanazotumia vijana wa sasa kuuza vitu mbalimbali, bidhaa, ikiwemo vipodozi vya akinamama huku wakiwa wanatembeza mitaani, ambapo miaka ya nyuma ni kazi zilizofanywa na watu wazima ambao walikuwa wanatembeza wakiwa wamebeba kapu lililotengenezwa kwa ukili.

Kazi zilizokuwa zinafanywa na wazee ni kama zimeboreshwa hivi na kuwa na kisasa zaidi kiasi cha kuwavutia vijana.

Enzi zile kinyozi alitumia mkasi na ofisi yake ni chini ya mti, ambapo kwa sasa kuna saluni inayotumia mashine za umeme.

Vijana hawatembei na kapu la ukili kuuza urembo, badala yake nao wameshajiongeza na kutengeneza mbadala wake, japo nao wameendelea kupita mitaani kwa miguu kama baba au babu zao.

**Tuma meseji 0716 350534**

HABARI KIMATAIFA

# Biden, Trump wachuana vikali kwenye mdahalo

**WASHINGTON,** MAREKANI

WAGOMBEA kiti cha urais nchini Marekani, Rais wa sasa Joe Biden na mpinzani wake Donald Trump, wamechuana vikali katika mdahalo wa kwanza wa uchaguzi.

Wakati wa mdahalo huo, kila mgombea alitafuta mbinu ya kumpiku mwenzake katika mbio za White House katika uchaguzi utakaofanyika Novemba mwaka huu.

Biden mwenye umri wa miaka 81, na Trump mwenye umri wa miaka 78, hawakusalimiana kwa kupeana mikono wakati walipo-simama jukwaani katika studio za makao makuu ya televisheni ya CNN yaliyopo katika jiji la Atlanta. Wakati wa mdahalo huo, hakukuwa na watazamaji ukumbini na vipaza sauti vilizimwa wakati kila mmoja alipokuwa akizungumza.

Rais Biden alifungua mdahalo kwa kumlaumu Trump kwa kuharibu uchumi ambao ulikuwa unaporomoka kwa kasi wakati alipochukua madaraka.

Alisema janga hilo lilishughulikiwa vibaya, watu wengi walikuwa wanakufa.

Trump alijibu kwa kuishambulia rekodi ya utawala wa Biden kwa kueleza haujafanya kazi nzuri na kusababisha hali ya mfumuko wa bei unaouwa nchi,Kiongozi huyo wa zamani wa taifa hilo kubwa, alitoa madai ya kuwa alikuwa bora katika mambo kadhaa, bila kutoa ushahidi.

Hata hivyo, Biden alionekana kutowaridhisha wanachama wa chama chake cha Democratic kutokana na sauti iliyofifia na wakati mwingine akionekana kupoteza mawazo yake.

**Gaza na Ukraine**

Mdahalo huo pia uliangazia sera ya kigeni hasa kuhusu vita vya Gaza na Ukraine.

Trump kwa upande wake alidai kuwa uungaji mkono wa Marekani kwa Ukraine unaumiza uchumi wa nchi hiyo.

"Hii ni vita ambayo haikupaswa kuanza kama tungekuwa na kiongozi katika vita hivi. Biden ametoa dola bilioni 200 mpaka sasa au zaidi kwa Ukraine, ametoa dola bilioni 200. Hizo ni pesa nyingi sana. Sidhani kama kuna kitu kama hicho kilishawahi kutokea," alisema Trump.

Hata hivyo, Biden alijibu kwa kueleza kwamba msaada wa kijeshi kwa Ukraine ulitolewa kwa njia ya silaha zilizotengenezwa na Marekani, ni sawa na mataifa mengine ya Magharibi yalivyochangia.

"Huyu ni mtu ambaye anataka kujiondoa katika NATO, nilipata mataifa mengine 50 kuisaidia Ukraine dhidi ya uvamizi wa Urusi," alisisitiza.

Uchaguzi huo unaweka historia kuwa wagombea hao wawili wa urais ndio wenye umri mkubwa zaidi kuwahi kuchaguliwa.

Wote waliulizwa maswali kuhusu uwezo wao wa kuwa rais kwa miaka mitano ijayo.

Akizungumza kwa sauti ya mkwaruzo kwa muda wote wa mdahalo, Biden alisema aliingia Bunge la Congress kama mmoja wa maseneta wenye umri mdogo zaidi kuwahi kutokea.

Aliendelea kupigia debe orodha ya mafanikio yake kama rais na akabainisha kuwa Trump ni mdogo wake kwa tofauti ya miaka mitatu pekee.


Katika majibu yake, Trump alidai alifaulu kwa urahisi vipimo vya utambuzi na kumwambia Biden naye akafanye vipimo hivyo.

Pia alijivunia uhodari wake wa kucheza gofu na kusema ana umbo zuri kama alivyokuwa miaka 25 iliyopita na labda sasa yeye ni mwepesi kidogo.

**Biden amtilia mashaka Trump**

Rais Biden alimshambulia Trump akitaka kuwakumbusha mamilioni ya watazamaji wa televisheni kuwa kama Trump atachaguliwa, atakuwa rais wa kwanza aliyehukumiwa kwa makosa. Hata hivyo, Trump alisema atakubali matokeo ya uchaguzi kama anafikiri yatakuwa ya haki.

**DW**



Rais Joe Biden na mpinzani wake Donald Trump wakishiriki mdahalo wa kwanza wa uchaguzi wa rais wa Marekani jana. **PICHA: REUTERS**

## Kenya yatawaliwa na utulivu

**NAIROBI,** KENYA

HALI ya utulivu imeanza kurudi katika mji mkuu wa Kenya, wa Nairobi na maeneo mengine ya nchi hiyo kufuatia maandamano yaliyofanyika juzi.

Biashara na maduka yamefunguliwa, huku wananchi wakiripotiwa kuendelea na shughuli zao za kawaida.

Maandamano hayo yaliyoongozwa na vijana wanaofahamika kama Gen-Z, yalianza wiki hii baada ya bunge la nchi hiyo kuupitisha mswada tata wa fedha uliotoa mapendekezo ya kuongeza kodi kwa mkate na mafuta ya kupikia.

Rais wa Kenya, William Ruto, alikataa kusaini mswada huo wa fedha kufuatia shinikizo la waandamanaji hao ambao waliingia bungeni na kuchoma moto baadhi ya majengo.

**DW**

# Serikali mpya Afrika Kusini hatarini kusambaratishwa

SIKU chache baada ya Afrika Kusini kuunda serikali ya umoja wa kitaifa, kuna madai ya kuwepo na mpasuko kati ya vyama washirika kuhusu nafasi za uongozi serikalini.

Vyama vikuu vinavyounda serikali hiyo ni African National Congress (ANC) na Democratic Alliance (DA) ambavyo vinalumbana kuhusu watu watakaoshika nafasi mbalimbali za madaraka.

Rais Cyril Ramaphosa, alimshutumu kiongozi wa chama cha DA, John Steenhuisen, kwa kujaribu kuunda serikali inayokiuka katiba.

Inasemekana alitoa madai hayo katika barua aliyomwandikia Steenhuisen Juni 25 , ambayo ilionekana na vyombo vya habari vya ndani ya nchi hiyo.

Kutokana na hali hiyo masoko ya hisa yamezorota kutokana na habari za kuongezeka kwa mpasuko.

Vyama vya ANC na DA vilitakiwa kugawana nyadhifa za baraza la mawaziri na kuanza kazi haraka.

Wakati ANC iliposhindwa kupata wingi wa kura katika uchaguzi wa mwezi uliopita, chama kikuu cha upinzani DA kilikubali kuunda serikali ya umoja wa kitaifa ambayo ilimweka Rais Ramaphosa madarakani.

Wanasiasa kutoka DA kupata nyadhifa.

Hapo awali, wachambuzi waliambia BBC kwamba pande hizo mbili zinaweza kuzozana wakati zitakapokuwa zikijaribu kufikia makubaliano, lakini mawasiliano ya hivi punde yaliyofichuliwa yanaashiria mpasuko ambao baadhi wanahofia huenda ukaathiri makubaliano ya muungano yaliyotiwa saini Juni 14, mwaka huu.

Taarifa za uwezekano wa kusambaratika kwa muungano huo ziliifanya thamani ya sarafu ya Afrika Kusini, rand, kuporomoka dhidi ya dola.

Wafanyabiashara walitetea makubaliano kati ya pande hizo mbili, wakiamini itasaidia nchi kufikia utulivu wa uchumi.

**BBC**

# MATUKIO KATIKA PICHA



Baadhi ya wakazi wa kisiwa cha Rukuba, Musoma Vijijini mkoani Mara wakiangalia mabaki ya mabati ya nyumba zao zilizoteketea kwa moto mapema wiki hii na kusababisha kaya 45 kukosa makazi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**



Ofisa Mipango wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali, mkoani Mbeya, Any-agile Mwanyamaki, akizungumza na watendaji wakati wa kikao kazi cha kujadili taarifa ya utekelezaji wa shughuli za Mradi wa Urejeshwaji Endel-evu wa Mazingira na Hifadhi ya Bioanuai Tanzania (SLR) kwa mwaka 2024, jijini Mbeya juzi. **PICHA: ISMAIL NGAYONGA**



Mkuu wa Mkoa wa Mara, Kanali Evans Mtambi (mwenye kofia), akiongo-zana na Mkuu wa Wilaya ya Bunda, Dk. Vincent Naano (wa tatu kushoto), wakati wakikagua ujenzi wa Shule ya Sekondari ya wasichana ya mkoa huo, inayojengwa eneo la Bulamba, wilayani humo, jana, kwa ajili ya maandalizi ya kupokea wanafunzi wa kidato cha tano. Wengine ni Mkuu wa shule hiyo, Nyaeri Mwisawa (kushoto), Katibu Tawala wa Mkoa huo, Gerald Kusaya (kulia) na msimamizi wa ujenzi wa shule hiyo, Mhandisi Timothy Mwanjala. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**



Mkuu wa Wilaya ya Muheza, mkoani Tanga, Zainab Abdallah (kushoto), akijadiliana jambo na Diwani wa kata ya Potwe, Athuman Bahari Papa, baada ya kumalizika kikao cha Naibu Waziri wa Maji, Mhandisi Kundo Mathew na madiwani wa Halmashauri ya wilaya hiyo, mapema wiki hii. Kulia ni Meneja wa RUWASA wa wilaya hiyo, Cleopha-ce Maharangata. **PICHA: STEVEN WILLIAM**



Meneja Mkuu wa kampuni ya uchimbaji madini ya Tanzanite ya Franone katika mji mdogo wa Mirerani, wilayani Simanjiro, mkoani Manyara, Vitus Ndakize (katikati), akizungumza kuhusu utafiti wa madini uliofanywa kwa kurusha ndege nyuki na Taasisi ya jiolojia na utafiti wa madini Tanzania (GST), kwenye kitalu C wanachokimiliki hivi karibuni. Kulia ni Mkurugenzi wa kampuni hiyo, Fransic Matunda. **PICHA: GIFT THADEY**

HADITHI

# HADITHI

TAARIFA ya Jeshi la Polisi inatangaza kuokotwa na maiti ya msichana mzuri na mrembo mno Mariamu, maeneo ya Tabata pembezoni mwa barabara mapema alfajiri. Alikuwa amevalia mavazi ya michezo. Alionekana alikuwa anakimbia, ametoka au anakwenda jogging. Taarifa ya madaktari inasema alikufa kwa mshtuko wa moyo, hiyo inaonyesha kuwa alianguka wakati anafanya zoezi alfajiri ile. Ndugu wa marehemu walikataa ripoti, kwani inaonekana kama alipigwa na kitu kizito kilichonasibishwa na chuma kichwani, kilichosabisha kuwa na tundu kichwani. Ndugu wanaliomba Jeshi la Polisi kufanya uchunguzi wa kina ili kugundua ukweli na wanaapa kuwa kama halikufanyika hilo, damu ya ndugu yao haitoenda bure. Kwani kuna nini? Kila nakala yako ya gazeti la Nipashe, itakupeleka kwenye ukweli wa jambo hili.

# Damu ya Mariamu-19

**Na Adam Fungamwango (0716 350534)**

Siku hiyo alipata makazi mapya. Ilikuwa maeneo ya kurasini kwenye mabehewa chakavu . Alipata ruhusu ya kulala hapo na walinzi wawili ambao waliwaambia alifika Dar kutoka Kigoma, lakini hakumkuta mwenyeji wake na alikuwa amezima simu.

Akawaambia kuwa hakuwa na chochote kile, chakula wala sehemu ya kulala. "Nilikuwa nawasiliana naye wakati nakuja Dar na yeye ndiye aliyeniambia nije, nashangaa kufika hapa kanizimia simu na hapatikani tena."

Walivyomuona, na jinsi alivyovaa, waliamini na kuamua kumkaribisha. Wakampa chakula na kumpa ruhusa ya kulala ndani ya moja ya mabehewa chakavu. Waliamini ndugu yake huyo anaweza kupatikana hewani baada ya siku chache, kwani huenda aliporwa na vibaka wakati anawasiliana naye.

Alichofanya Kamal, ni kutoka na kibegi chake kwenye hospitali aliyokuwa kama amekodi ambayo alilala kwa siku kadhaa, akaenda kuoga na kubadilisha nguo zake katika bafu moja pale, Ilala Karume nje ya Shirikisho la Mpira wa Miguu Nchini (TFF), akavaa nguo zilizomfanya awe na muonekana kama mtu aliyechoka hivi, fukara, masikini, hana kitu, mchovu, ndipo alipokwenda maeneo ya Kurasini ambako, baadhi ya vichwa vya treni na mabehewa hufanyiwa matengenezo.

Alichowaza ndicho kilichotokea, nia yake ilikuwa ni kulala kwenye mabehewa mabovu ambayo hayatumiki tena. Lakini ilikuwa ni lazima kuwakabili walinzi kwa uongo. Akafanikiwa. Nia ilikuwa ni kutoendelea kuishi tena hospitalini kwa ajili ya usalama. Alitaka kuwasiliana na dokta Shija akiwa haishi tena hapo.

**********************************

Alijizoazoa kutoka kwenye moja ya kiti cha behewa bovu na chakavu, akashuka chini. Tayari alishakuwa hapo kwa siku tatu. Walinzi walishaanza kumzoea na kumtania jinsi alivyoachwa solemba na mwenyeji wake.

Hata hivyo wapo waliowaambia walinzi kuwa makini na mtu huyo kwani huenda ni mpelelezi. Hiyo ilifanya washindwe hata kumuambia aondoke. Wakamuacha tu akiendelea kuwa hapo. Pamoja na yote, walimpenda kutokana na kuwa mcheshi na akirejea wakati mwingine anawaletea zawadi za vyakula kama mihogo, viazi, mahindi ya kuchoma au kuchemsha.

Simu yake iliita. Aliingiza mkono mfukoni na kuitoa. Jina lilisomeka dokta Shija. Akaiweka sikioni kwa makini.

"Hallo kijana, njoo hapa Kariakoo, kwenye Makutano ya Uhuru na Msimbazi, kuna mazungumzo kidogo nataka tuongee. Nadhani haya yanaweza kukusaidia katika ule mpango wako, sawa?" "Sawa." Akajibu Kamal.

Hata hivyo wasiwasi ukaanza kumuingia Kamal. Kama kawaida yake ya kutia shaka kwa kila jambo.

Je ni kweli dokta ananiitia hilo, au anataka kwenda kunikamatisha? Je ameshawaambia madaktari wenzake ambao wamemwambia achana naye, na kufanya mpango wa kumkamata, au kumuua ili kupoteza ushahidi?" Akajiuliza.

Akavuta kumbukumbu baadhi ya vitabu alivyosoma ni kwamba baadhi ya wapelelezi huamua kujitoa muhanga ili kuelekea karibuni ya ukweli.

Wanalazimika kugatarisha maisha yao ili kuwa karibu na wahalifu, na hii ni kutaka kujua ukweli wa mksa mzima kwani wanakuwa mikononi mwa maadui.

Pia kwa jinsi alivyoongea Dokta Shija kwenye simu, hakuonekana kama mtu anayetaka kumfanyia lolote baya, kwa sababu hata uongeaji wake ulikuwa wa uangalifu. Alionekana kuongea na umakini bila kumtaja jina, au kuelekeza kitu ambacho wanataka kwenda kuongea.


Hiyo pia ilimpa moyo kuwa huenda hakuna lolote baya litakalomkuta. Uwezo wake wa kujilinda, kuwa na uwezo wa sanaa za mapigano, pia ulimfanya ajiamini. "Nitakwenda" Akajiambia.

Hakutumia muda mrefu sana. Kutoka Kurasini mpaka alipoitwa, makutano ya barabara za Uhuru na Msimbazi hakukuwa mbali sana.

Alisimama pembeni kidogo akiwa amejificha ili iwe rahisi kumuona yoyote ambaye anamsaka. Ghafla aliliona gari lenye rangi kijivu, aina ya Toyota Fortuner, lilisimama pembeni na akashuka mtu ambaye anamfahamu.

Ni dokta Shija. Akaangalia huku na huku. Alikuwa peke yake. Kamal alisubiri kidogo mpaka alipohakikisha kuwa hakuna mtu mwingine anayewasiliana naye, na hata ndani ya gari hakuna mtu.

Akamuona akaingiza mkono mfukoni, akajua kabisa kuwa anatoa simu ya mkononi. Akaondoka haraka na kwenda mbali ili ikiita asisikie. Akavuka barabara kuelekea kama anakwenda kwenye klabu ya Simba.




**Akaufuata mlango. Dokta alipofungua ule wa dereva na yeye akafungua. Hakupanda kwanza, akaangalia siti ya nyuma na upande wake wa pili.**

Macho na akili yake bado ilikuwa na dokta. Alijua kama hampigii yeye basi kuna mtu mwingine atakuwa anampigia. Na hatokuwa mtu mzuri kwake. Kama atapigiwa yeye basi ataamini hakuna tatizo lolote.

Simu ikaita, akapokea "Uko wapi wewe?" Dokta akauliza. "Nipo karibu tu hapa, nilitoka tu kidogo kuangalia vitu hapa, lakini nilishafika hapo." Muda huo huo, alikuwa ameshafika eneo hilo, na Dokta Shija akamuona.

"Mimi nadhani si vizuri haya tutakayoongea yasikike na watu wengine. Tuingie ndani ya gari.

Humo tutakuwa wawili tu, tutaongea vizuri." "Poa" Akaitikia Kamal.

Akaufuata mlango. Dokta alipofungua ule wa dereva na yeye akafungua. Hakupanda kwanza, akaangalia siti ya nyuma na upande wake wa pili.

Alipohakikisha kuwa hakuna mtu mwingine akapanda. Hilo lilimvutia dokta Shija, akamuuliza "Wewe umeshawahi kuwa askari halafu ukafukuzwa nini?" "Kwa nini dokta?" "Mmmh! Yaani unaonekana uko makini sana, muangalifu sana, halafu una tekniki zile zile, tena siyo askari wa kawaida." "Hapana, kawaida tu."

"Unajua nini, hata ulipokuja kwenye zahanati yangu, mbinu uliotumia hadi tukakupa kitanda ukakaa pale wiki mbili.

Sidhani kama kuna mtu anaweza kuwa na akili kama hiyo ya kuishi hospitalini ambapo hakuna askari anayeweza kumtafuta mhalifu. Halafu uliponifahamisha tu kuwa wewe ndiye yule unayetafutwa kwa kumuua mpenzi wako, ukahama pale, hukulala tena pale, hizo zote ni mbinu za kipelelezi tu."

Dokta Shija akafunguka. Maneno hayo yalimfanya Kamal kuangua kicheko. Hakujibu kitu. "Tuyaache hayo.

Kuna kitu ambacho nimekipata kwa ile kazi uliyonituma, haoa ndani ya gari itabidi tuzunguke tu, twende mpaka Buruguni, tukate mpaka Tabata, Ubungo, Magomeni, turudi Ilala Boma mpaka hapa hapa tena Kariakoo nikuteremshe, nadhani mazungumzo yatakuwa yamekamika, nitakuwa naendesha taratibu."

Kamal alikuwa amekaa kimya na makini alimsikiliza Dokta Shija ni kitu gani ambacho ataka kumwambia ambacho kinaweza kumpa mwangaza wa nani yupo nyuma ya mauaji ya mpenzi wake, Mariamu hadi yeye kusingiziwa kuwa ndiye alimuua?

**Itaendelea Jumamosi**

# COASTAL UNION YATUA KWA MUKOKO TONOMBE

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Coastal Union inatajwa ipo kwenye mazungumzo na kiungo mkabaji wa zamani wa Yanga, Mukoko Tonombe kwa ajili ya kuiongezea nguvu katika michuano ya Kombe la Shirikisho barani Afrika.

Chanzo kutoka ndani ya klabu hiyo kinasema kuwa mazungumzo yanaendelea vyema na kama yakikamilika, mchezaji huyo ambaye amemaliza mkataba wake na TP Mazembe ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, atavaa uzi mwekundu na mweupe.

Mukoko ambaye yupo nchini, mwenyewe akidai kupumzika na kusalimia ndugu wa mkewe, aliichezea Yanga mwaka 2020 hadi 2022 akisajiliwa kutoka AS Vita ya kwao, na aliachana na timu hiyo akajiunga na TP Mazembe 2022 hadi mkataba wake ulipomalizika mwaka huu.

Alipoulizwa kuhusu tetesi hizo, Ofisa Habari wa Coastal Union, Abbas El Sabri hakukataa wala kukubali, badala yake akawataka mashabiki wa klabu hiyo kuwa watulivu kwani kuna wachezaji wengi bora wa kigeni ambao wataichezea timu hiyo msimu ujao.

"Siyo Mukoko tu unayemsema, kuna wachezaji wengi wa kimataifa wazuri tu ambao tunazungumza nao, hivi ninavyokwambia kuna beki wa timu ya taifa ya Uganda yupo nchini kwa ajili ya kukamilisha usajili na Coastal Union, siwezi kutaja jina lake kwa sasa kwani hiki ni kipindi cha usajili na kuna timu kazi yao ni kuchukua tu wachezaji wanaoletwa na klabu zingine," alisema.

El Sabri alisema beki huyo wa kati amekuja kuchukua nafasi ya Fally Mulumba, raia wa Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo ambaye wameachana naye.

Mbali na Mukoko, Coastal ambayo ilikiri iko kwenye mazungumzo na beki wa kulia za zamani wa Yanga, Djuma Shaaban, pia inadaiwa kutaka kuwasajili Tuisila Kisinda aliyemaliza mkataba wake RS Berkane ya Morocco na Mrundi, Saido Ntibazonkiza aliyemalizana na Simba.

MAZOEZI



Vijana wakifanya mazoezi ya mpira wa miguu katika viwanja vya Jakaya Kikwete jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## Moto wa 'Dar Boxing Day' kuwaka leo

**Na Shufaa Lyimo**

MABONDIA mbalimbali watakaoshiriki pambano la ngumi la ,Dar Boxing Day' linalotarajiwa kufanyika leo kwenye viwanja vya Posta, Kijitonyama jana walipima uzito tayari ,kuwasha moto' kwenye pambano hilo litakalohusisha mabondia mbalimbali.

Akizungumza na Nipashe jana, msimamizi wa pambano hilo, Emanuel Mlundwa, alisema watachukua hatua kali kwa bondia ambaye atavunja kanuni na taratibu za pambano hilo.

"Tutachukua hatua kali kwa yeyote ambaye atavunja kanuni na taratibu za pambano hili ili iwe fundisho kwa wengine," alisema Mlundwa.

Aidha, alisema waandaaji hawatamuonea huruma atakayekiuka taratibu hizo kwa kuwa wapo kwa ajili ya kuhakikisha mchezo wa ngumi unazidi kukua.

Kwa upande wake muandaaji wa pambano hilo, Meja Selemani Semunyu, alisema maandalizi yote yamekamilika na kuwataka wadau wa mchezo huo wajitokeze kwa wingi kushuhudia burudani kutoka kwa mabondia mbali mbali.

"Ninaomba watanzania waje kwa wingi kushuhudia burudani zitakazoonyeshwa na mabondia wetu, vile vile ninaahidi kushirikiana na yeyote mwenye nia ya kujifunza mchezo huu," alisema Meja Semunyu.

Wakati huo huo, bondia Juma Choki ambaye atapigana na Nassib Ramadhani alimpa tahadhari mpinzani wake huyo kwa kusema atampa kichapo kikali ili arudishe heshima yake.

"Nitampa Nassib kichapo kikali ambacho hajawahi kukipata, ninaomba mashabiki wangu mjitokeze kwa wingi kesho (leo) kuona burudani nitakayoionyesha, alisema Choki.

# KVZ yajitetea kuukosa ubingwa Zanzibar

**Na Hawa Abdallah,**
ZANZIBAR

TIMU ya KVZ FC imesema kushindwa kupata ubingwa msimu uliomalizika wa Ligi kuu ya Zanzibar hivi karibuni kumechangiwa kwa kiasi kikubwa kuwakosa wachezaji wao watano muhimu katika mzunguko wa pili.

Wachezaji hao watano hawakuwepo kwenye kikosi hicho kutokana na majukumu kwa kuwa walikuwa kwenye kozi jeshini.

KVZ FC imemaliza nafasi ya nne katika msimamo wa Ligi kuu ya Zanzibar kwa msimu ulioisha wa 2023/2024.

Timu hiyo katika michezo 30 waliyocheza walishinda michezo 17, wakitoka sare michezo mitano na kufungwa michezo nane.

Akizungumza na gazeti hili Ofisa habari wa timu hiyo, Hussein Mohamed alisema dhamira yao kubwa ya kutwaa ubingwa kwa misimu miwili mfululizo haikufanikiwa licha ya msimu huu kushindwa kufanya hivyo katika hatua za mwishoni.

Alisema hapo awali timu hiyo ilianza msimu vizuri lakini baada ya wachezaji wao kuondoka kuelekea katika mafunzo ndio iliyopelekea kutibuka kwa mpango huo.

Alisema ingawa waliwakosa wachezaji hao tegemeo katika kikosi cha kwanza lakini wachezaji waliosalia walipambana mpaka kumaliza Ligi katika nafasi ya nne.

"Tulianza msimu kwa malengo ya Ubingwa, na lengo letu tulienda nalo mpaka michezo ya mwisho ya Ligi pale tulipotoka katika mbio hizo baada ya kupoteza michezo kadhaa muhimu" alisema, Mohamed.

Aidha alisema kuwa kwa ujumla msimu wa 2023/2024 ulikuwa msimu mgumu na wenye ushindani mkubwa ndio maana hata bingwa kapatikana katika mchezo wa mwisho wa kufunga panzia la Ligi hiyo.

Hata hivyo alisema uongozi wa timu wanasubiri ripoti ya benchi la ufundi ili kujua mapendekezo yao kuelekea maandalizi ya msimu ujao wa Ligi Kuu ya Zanzibar.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### LIVERPOOL YAMSAKA GULER
LIVERPOOL inamfuatilia kiungo mshambuliaji wa Uturuki mwenye umri wa miaka 19, Arda Guler kutoka Real Madrid (***Teamtalk***)

### TREVOH CHALOBAH AWANIWA
KLABU ya Fulham imefufua nia yao ya kumnunua beki wa Chelsea mwenye umri wa miaka 24,Trevoh Chalobah. (***Standard***)

### MAN KUMTOSA BRANTHWAITE
KLABU ya Manchester United itaachana na mazungumzo na Everton kwa ajili ya kumnunua beki, Jarrad Branthwaite mwenye miaka 21, endapo The Toffees hawatapunguza bei yao ya pauni milioni 70. (***ESPN***)

### YORO ANAITAKA REAL MADRID
MLINZI wa Lille, Leny Yoro mwenye miaka 18, anapendelea kuhamia Real Madrid badala ya Liverpool au Manchester United . (***Marca***)

### KUDUS KUOMBA KUONDOKA
KLABU ya West Ham inahofia winga wa Ghana, Mohammed Kudus mwenye miaka 23, ataomba kuondoka katika klabu hiyo msimu huu wa majira ya joto. (***Football Insider***)

### A' VILLA YAMUULIZIA SOULE
ASTON Villa imeuliza kuhusu uwezekano wa kumsajili kiungo wa kati wa Argentina, Matias Soule mwenye miaka 21, lakini Juventus inasema hauzwi. (***Sky Sports***)

### ANSELMINO ATAKIWA CHELSEA
CHELSEA ipo kwenye mazungumzo na Boca Juniors kuhusu dili la kumnunua beki wa Argentina mwenye miaka 19, Aaron Anselmino. (***Athletic***)

### ZIRKZEE ANYATIWA MAN U
KLABU ya Manchester United inajiandaa kutumia kipengele cha kuachiliwa kwa pauni milioni 33.8 katika mkataba wa mshambuliaji wa Bologna Mholanzi Joshua Zirkzee mwenye miaka 23. (***Telegraph***)

### BAYERN YAMTAKA NYOTA WA PSG
KIUNGO wa kati wa Paris St-Germain na Uholanzi, Xavi Simons mwenye umri wa miaka 21, ndiye anayelengwa zaidi na Bayern Munich ya Ujerumani. (***Bild*** )

### PIOLI ATAJWA KUINOA AL-ITTIHAD
KOCHA wa zamani wa AC Milan, Stefano Pioli ni miongoni mwa wanaowania kuwa kocha wa Al-Ittihad . (***Fabrizio Romano***)

### KADIOGLU ATAKIWA ARSENAL
ARSENAL imewasilisha ombi la kumnunua beki wa pembeni wa Fenerbahce, Ferdi Kadioglu mwenye umri wa miaka 24. (***Ajan Spor***)




# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# MARC GUEHI: ENGLAND HAIJAPATA MCHEKEA

**Nyota huyo amesisitiza licha ya kukwepa kukutana na vigogo, bado ina kazi kubwa ya...**

**BERLIN,** Ujerumani

Marc Guéhi amesisitiza "hakuna upande mzuri wa droo" baada ya England kuziepuka Ufaransa, Hispania, Ujerumani na Ureno katika njia yao ya kuelekea fainali ya Euro 2024.

Kikosi cha Gareth Southgate kitamenyana na Slovakia katika mchezo wa hatua ya 16 bora Jumapili mjini Gelsenkirchen baada ya kumaliza kileleni mwa Kundi C kwenye michuano hiyo inayofanyika Ujerumani.

Alipoulizwa maoni yake kuhusu kupangwa na Slovakia, Guéhi aliuambia mkutano wa waandishi wa habari, „Kuhusu droo, nadhani kila mtu ameona katika fainali hizi kwamba sidhani kama kuna timu nyepesi kwa michuano hii.

"Kila timu, kila mpinzani unayekutana naye ni mgumu sana kucheza naye. Lakini nadhani tunatakiwa kuwa watulivu. Hayo ndiyo mazingira tunayojiwekea. Tunajipa presha lakini ni mazingira tulivu na yenye umakini.

> **"Hatujafanya uchambuzi wowote wa timu juu yao [Slovakia] lakini sote tuna tazama michezo na tunajua ni timu nzuri sana. Walishika nafasi ya tatu kwenye kundi na kufuzu.**

Wana wachezaji wazuri sana upande wao, (Stanislav) Lobotka akiwa mmoja wao, dhahiri kutoka Napoli na wengine wazuri kwenye kikosi chao.

"Itakuwa changamoto nyingine ngumu kukabiliana nayo. Lazima tuwe tayari kwa changamoto hizo na kukabiliana na upinzani wowote watakaotuonyeshea. Kinachojenga kujiamini ni umoja, utendaji, ukweli kwamba bado hatujapoteza mchezo jambo ambalo ni muhimu sana.

"Vitu vingine vyote hatuwezi kuvidhibiti. Nadhani ni muhimu tu kudhibiti kile tunachoweza kudhibiti, hiyo ni kubaki watulivu, makini na kukabiliana na vikwazo vyovyote vilivyo mbele yetu."

Guéhi, ambaye bila shaka amekuwa mchezaji bora wa England kwenye Euro 2024, pia alimtetea Southgate kutokana na ukosoaji wa hivi majuzi wa uchezaji wa England huku baadhi ya mashabiki wakimzomea na kumrushia vikombe vya bia baada ya sare ya 0-0 Jumanne na Slovenia.

## HABARI MICHEZO

# SANCHO, GREENWOOD WATARAJIWA KURUDI UNITED

**MANCHESTER,** England

MANCHESTER United inatarajia Jadon Sancho na Mason Greenwood watarejea mazoezini ikiwa hawataondoka kwenye klabu hiyo katika kipindi hiki cha usajili, chanzo kimeiambia ESPN.

United imewaambia wachezaji ambao hawajashiriki michuano ya Ulaya au Copa America kurejea Carrington Julai 8.

Klabu hiyo inajitahidi kutafuta klabu mpya kwa Sancho na Greenwood, lakini ikiwa watasalia kuwa wachezaji wa United kufikia tarehe hiyo ya mwisho watatakiwa kurejea mazoezini.

Greenwood, ambaye anasakwa na Lazio, Juventus, Napoli na Marseille, anaweza kufanya mazoezi Carrington kwa mara ya kwanza tangu Januari 2022, aliposimamishwa kutokana na tuhuma za ubakaji.

Greenwood alianza tena uchezaji wake kwa mkopo Getafe msimu uliopita.

Chanzo kiliiambia ESPN kwamba mipango ya kurudi kwa Sancho bado haijakamilika.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24, ambaye alitumia kipindi cha pili cha msimu uliopita kwa mkopo katika klabu ya Borussia Dortmund, hajafanya mazoezi na kikosi cha kwanza tangu kutofautiana kwake na kocha, Erik ten Hag, Septemba.

Vyanzo vimeiambia ESPN kwamba Sancho amepewa ofa kwa Barcelona na Juventus, lakini thamani ya takriban pauni milioni 40 ni kikwazo kwa klabu zinazovutiwa nae.




# Nguemo wa Cameroon afa ajalini



**YAOUNDE,** Cameroon

KIUNGO wa zamani wa Celtic na Bordeaux, Landry Nguemo alifariki katika ajali ya gari katika nchi yake ya asili, Cameroon siku ya Alhamisi akiwa na umri wa miaka 38.

Shirikisho la Soka la Cameroon limethibitisha habari hiyo kupitia taarifa yake.

„FECAFOOT tunatoa pole kwa kifo cha aliyekuwa nyota wa Cameroon, Landry Nguemo kufuatia ajali ya barabarani. „FECAFOOT tunatoa pole kwa familia yote ya soka," ilisema taarifa hiyo.

Kiungo huyo mlinzi alijipatia jina katika soka la Ufaransa akiwa klabi ya AS Nancy, ambapo alikuwa mshindi wa Kombe la Ligi mwaka 2006 na alitumia muda kwa mkopo Celtic kabla ya kuhamia Bordeaux kabisa mwaka 2011.

Alikaa miaka mitatu Les Girondins kabla ya kucheza Saint-Etienne na baadae Uturuki akiwa na Akhisar Belediyespor na Kayserispor.

Alimaliza soka lake mwaka 2019 kufuatia kucheza muda mfupi kwenye klabu ya Kongsvinger ya Norway.

Kati ya 2006 na 2014, Nguemo aliichezea Cameroon mechi 41, akiiwakilisha katika michuano miwili ya Kombe la Mataifa ya Afrika.

Alikuwa mchezaji wa akiba ambaye hakutumiwa katika mechi ya fainali ya 2008 dhidi ya Misri mjini Accra, Ghana.

Tangu kustaafu, alifundisha timu ya vijana ya AS Nancy na pia aliwekeza katika nchi yake.

# Argentina kumpumzisha Lionel Messi

**MIAMI,** Marekani

LIONEL Messi hatacheza mechi ya mwisho ya hatua ya makundi ya michuano ya Copa América 2024 dhidi ya Peru kwenye Uwanja wa Hard Rock huko Miami, Florida leo Jumamosi usiku, vyanzo viliiambia ESPN Argentina.

Messi alipata jeraha wakati wa mechi dhidi ya Chile Jumanne usiku na alitibiwa nje ya uwanja katika kipindi cha kwanza.

Alithibitisha baada ya mechi kwamba alihisi maumivu kwenye msuli wake wa kulia, lakini aliweza kuendelea kucheza.

Siku ya Alhamisi alasiri, nyota huyo mwenye umri wa miaka 37 alibaki katika hoteli ya timu na hakwenda Chuo Kikuu cha Kimataifa cha Florida kwa mazoezi ya Argentina.

„Nilihisi maumivu katika msuli wa paja wa kulia mwanzoni mwa mchezo. Ulikuwa umebana. Lakini niliweza kumaliza mchezo. Tutaona jinsi itakavyokuwa, „ alisema Messi katika mahojiano na vyombo vya habari.

Kocha wa Argentina, Lionel Scaloni alisema baada ya mechi ya Chile kuwa anatarajia kufanya mabadiliko kadhaa kwenye kikosi cha kwanza dhidi ya Peru na kuwapa wachezaji wachanga fursa ya kupata muda wa kucheza uwanjani.


Kocha huyo aliyeshinda Kombe la Dunia alisema: „Tumeridhika, na tunaweza kufurahia siku na kuwapa wale walio na umri mdogo dakika zaidi.

Nadhani ni haki kuwa na wachezaji ambao hawakuwa na dakika kuingia uwanjani."

Exequiel Palacios, Guido Rodríguez, Valentin Carboni na Alejandro Garnacho bado hawajaichezea Argentina wakati wa michuano hiyo licha ya kushiriki mechi za kirafiki za kabla ya Copa America dhidi ya Guatemala na Ecuador.

Vyanzo vya habari viliongeza kuwa Garnacho ni mmoja wa wachezaji ambao wana uwezekano mkubwa wa kuingia uwanjani dhidi ya Peru.

Argentina haitegemei matokeo ya mchezo wa Peru ili kufuzu kwa raundi ya mtoano ya michuano hiyo.



## HABARI MICHEZO

## *Simba Day kuvunja rekodi msimu huu*

INATOKA UK. 24

Alisema mashabiki wa timu hiyo watapata ‚suprise' mbalimbali katika usajili wa timu hiyo msimu huu huku pia wakipanga kuwa na burudani za aina yake zitakazowafurahisha mashabiki wao.

Tamasha hilo litakuwa la 25 kwa klabu hiyo kubwa tangu walipobuni na kulifanya kwa mara ya kwanza mwaka 2009 chini ya Mwenyekiti wa Klabu hiyo wakati huo, Hassan Dalali, ambapo sasa imekuwa ni utamaduni wao kufanya tamasha hilo.

Miaka michache baada ya kuanzisha tamasha hilo, klabu nyingine nazo zilianza kufanya matamasha yao.

Katika tamasha la kwanza mwaka 2009, Simba ilicheza mechi kirafiki na klabu ya SC Villa ya Uganda kwenye Uwanja wa Uhuru na ikashinda bao 1-0 lililofungwa na Hilary Echessa, kiungo wa Kenya aliyekuwa amesajliwa msimu huo, timu ikiwa chini ya kocha Mzambia, Patrick Phiri.

Ni msimu huo Simba ilikuwa imewasajili kwa mara ya kwanza wachezaji wawili raia wa Uganda, Emmanuel Okwi na Joseph Owino.

Tamasha la msimu uliopita lilifanyika Agosti 6, Uwanja wa Benjamin Mkapa Simba ikicheza dhidi ya Power Dynamos ya Zambia na kupata ushindi wa mabao 2-0 yaliyowekwa wavuni na Willy Onana na Fabrice Ngoma ambao nao walikuwa wachezaji wapya katika kikosi hicho.

## Yanga SC yafunga usajili mpya, Pacome kuongezwa mkataba

INATOKA UK. 24

kiungo mshambuliaji, Pacome raia wa Ivory Coast ambaye kwa siku za karibuni amekuwa akihusishwa kutimkia klabu za FAR Rabat ya Morocco na Kaizer Chiefs ya Afrika Kusini.

Ingawa Pacome ana mkataba wa mwaka mmoja zaidi wameamua kukaa naye ili wampe mkataba mwingine ili kuhakikisha anasalia kwa muda mrefu ndani ya timu hiyo.



# AZAM YAKANA KIPRE KUTAKA KUONDOKA

**Na Faustine Feliciane**

LICHA ya kuibuka tetesi za mchezaji wake Kipre Junior kuhusishwa kutakiwa na klabu ya USM Alger ya Algeria, uongozi wa Azam FC umesema haujapokea ofa yoyote inayomuhusisha mchezaji huyo.

Aidha, wameenda mbali na kudai wapo katika kuboresha kikosi chao kwa ajili ya Ligi ya Mabingwa Afrika na hawataruhusu wachezaji wao tegemezi kuondoka.

"Hiki ni kipindi cha usajili, tetesi nyingi zitasikika, kuhusu Kipre huyu bado ni mchezaji wetu na tupo kwenye malengo yetu msimu ujao," alisema Zaka Zacharia, Ofisa habari wa klabu hiyo alipoulizwa juu ya tetesi hizo.

Hata hivyo alisema soka ni biashara kama kuna timu inamtaka mchezaji huyo au mchezaji mwingine yeyote basi wawasilishe ofa zao kwa uongozi.

**"Kama kuna timu in amtaka Kipre basi wa natakiwa kuwasiliana na Azam FC, mpaka sasa tunapoongea hakuna ofa yoyote ya ndani au nje ya nchi inayomtaka mchezaji huyu, hizo ni tetesi tu," alisema Zaka.**

Aidha, alisema Azam hawatakuwa tayari kuruhusu wachezaji wake tegemeo waondoke kiragiisi kwa kuwa malengo yao ni kuhakikisha wanafanya vizuri kwenye michuano ya kimataifa msimu ujao.

Msimu ujao Azam FC itaungana na Yanga kuiwakilisha nchi kwenye michuano ya Kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika baada ya kumaliza ligi kwenye nafasi ya pili.




KLABU ya Azam FC imemtambulisha Mbrazil, Romulo De Oliveira Freitas (kushoto) kuwa Mtaalamu wake mpya wa Matibabu ya Viungo kwa Wachezaji wake kwa mkataba wa mwaka mmoja, kulia ni Ofisa Mtendaji Mkuu wa klabu hiyo, Abdulkarim Amin 'Popat' baada ya kusaini mkataba huo. **PICHA: BINZUEIRY**

# Yanga kuuma na Safari Champion

**Na Shufaa Lyimo**

KIKOSI cha mabingwa wa soka nchini, Yanga leo kitashuka kwenye uwanja wa Benjamin Mkapa kupimana ubavu na kikosi cha Safari Champion katika mchezo maalum kwenye uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Mchezo huo unaosubiriwa na mashabiki mbalimbali umepangwa kuchezwa kuanzia saa 2:15 usiku.

Kikosi kinachokutana na Yanga ni kile ambacho kilipatikana kupitia programu maalum iliyoendeshwa na TBL ambayo ilitafuta vijana wenye vipaji kutoka mikoa mbali mbali na kufanikiwa kuunda timu yenye wachezaji 25.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, Kocha Mkuu wa timu ya Vijana ya Yanga, Soud Slim anayesimamia kikosi cha Yanga, alisema wamejiandaa vema kuhakikisha wanapata ushindi katika mchezo huo ambao utakuwa na upinzani mkubwa kutokana na uwezo wachezaji wanaounda kikosi cha Safari Champion.

"Timu ya Safari Champion ni timu yenye ushindani kutokana na aina ya wachezaji waliopo ndani ya kikosi hicho, baadhi nimeona wana uwezo mkubwa sana na wataweza kutoa upinzani kwa kwetu, alisema Slim.

Aidha aliwataka watanzania wajitokeze kwa wingi uwanjani hapo kushuhudia mchezo huo.

Kwa upande wake, Kocha Mkuu wa timu ya Safari Champion, Sekilojo Chambua, alisema amewajenga kisaikolojia wachezaji wake ili waweze kuonyesha viwango vyao katika mchezo huo.

"Nimewajenga kisaikolojia wachezaji wangu kuhakikisha wanafanya vizuri licha ya kuwa hawajawahi kucheza michezo ya usiku," alisema Chambua.

Alisema maandalizi ya siku 26 aliyoyafanya anaamini yatawasaidia kwa kiasi kikubwa kuonyesha vipaji vyao kupitia mchezo huo.

# Michezo

Jumamosi Juni 29, 2024

**Nipashe**




## Guehi: England haijapata mchekea

UK. 21



Mchezaji wa klabu ya PSG ya Ufaransa na timu ya taifa ya Morocco, Archraf Hakim (kulia) akipokea zawadi kutoka kwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Maliasili na Utalii, Hassan Abbas baada ya kuitembelea Tanzania katika kipindi hiki cha mapumziko. **PICHA: BINZUBEIRY**

# Simba Day kuvunja rekodi msimu huu

**Na Mwandishi Wetu**

## ●●● Uongozi watangaza tarehe rasmi ya tamasha hilo, yapanga kuvunja rekodi na kuwashangaza mashabiki utambulisho wa....

UONGOZI wa klabu ya Simba umetangaza rasmi siku ya kilele cha tamasha lake la kila mwaka maarufu ‚Simba Day‘ ambapo msimu huu limepangwa kufanyika Agosti 3 kwenye uwanja wa Benjamin Mkapa huku wakipanga kuvunja rekodi za matamasha yaliyopita.

**Klabu hiyo itatumia tamasha hilo kuwapa ‚suprise‘ mashabiki wao kwenye utambulisho wa wachezaji wao wapya watakaounda kikosi cha timu hiyo kwa ajili ya msimu ujao.**

Akizungumza jijini Dar es Salaam jana, Meneja Habari na Mawasiliano wa Klabu hiyo, Ahmed Ally, alisema kilele hicho kitafuatiwa na wiki nzima ya wanachama na mashabiki kufanya kazi za kijamii maeneo mbalimbali nchini kabla ya wote kujumuika Uwanja wa Mkapa kwenye siku ya kilele, ingawa hakutaja timu ambayo itacheza na kikosi hicho.

Tamasha hilo la kila mwaka linawakutanisha wanachama na mashabiki wa Simba ambao pamoja na mambo mengine ya burudani ya muziki na ngoma kutoka kwa wasanii mbalimbali pia kutakuwa na mechi za timu za vijana na za wanawake. Pia kutumia tamasha hilo kutangaza kikosi kipya kwa ajili ya mashindano mbalimbali na baadae kumaliza tamasha hilo kwa mchezo wa kimataifa wa kirafiki kati ya kikosi cha Simba na timu alikwa.

"Tungependa kutoa taarifa kwa Wanasimba wote kuwa tarehe rasmi ya tukio letu kubwa la Simba Day itakuwa Agosti 3 mwaka huu, Uwanja wa Benjamin Mkapa hapa hapa Dar es Salaam.

"Tumeamua kutangaza mapema ili watu wanaokuja kutoka mataifa mbalimbali ya nje waanze kukata tiketi mapema, unajua Simba Day huwa inaleta watu kutoka maeneo mengi duniani, ikumbukwe msimu uliopita tiketi ziliisha siku mbili kabla ya kilele chake, haijawahi kutokea, sasa safari hii tunataka rekodi ivunjwe," alisema Ahmed.

INAENDELEA UK. 23

## Yanga SC yafunga usajili mpya, Pacome kuongezwa mkataba

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI uongozi wa klabu ya Yanga ukijiandaa kumuongezea mkataba kiungo mshambuliaji wake Pacome Zouzoua, umetangaza kukamilisha na kufunga usajili wake msimu huu na sasa wanasubiri kuwatangaza rasmi wachezaji wote waliowasajili.

Rais wa Klabu hiyo, Hersi Said amesema jana kuwa tayari wameshamaliza usajili na sasa vimebaki vitu vichache ikiwemo Idara ya Habari kuweka utaratibu ili waanze kuwaweka hadharani.

„Tupo makini, kazi kubwa tumeshaifanya, tumeshasajili na karibuni asilima 99 kazi imekwisha, hivi sasa tumeiachia tu Idara ya Habari kutengeneza njia nzuri ya kutambulisha wachezaji wote tuliowasajili," alisema Hersi.

Alisema katika usajili wao wamejikita tu kwenye maeneo ambayo wanaona yana mapungufu na si vinginevyo.

„Suala la usajili huu ndiyo wakati wake na ni muhimu sana kuliko wakati mwingine wowote, ni kipindi cha kutuliza akili ili kupata wachezaji wazuri.

Sisi Yanga kuna maeneo ambayo tumelazimika kuyaboresha kwenye kikosi chetu ili kuwa bora zaidi, kwa hiyo nichukue fursa hii kuwaambia wana Yanga wawe tayari kuanzia tarehe moja Julai tutaanza kuelezea, au kutoa taarifa za usajili za wachezaji wetu wapya, wale tunaowaongezea mikataba na tutakaowaacha," alisema Hersi.

Wachezaji wanaohusishwa kutua kwenye klabu hiyo ni Wakongomani watatu, beki wa kushoto, Chadrack Boka kutoka FC Lupopo, kiungo mkabaji, Agee Basiala wa klabu ya Maniema Union na winga Emmanuel Lobota anayeichezea Singida Black Stars.

Mchezaji mwingine anayetajwa ni Chikamso Okechukwu, beki wa kati kutoka klabu ya Enyimba.

Wakati huo huo, klabu hiyo imesema ipo kwenye mazungumzo ya kumuongeza mkataba

HABARI UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >